PARLIAMENT OF TANZANIA · BUNGE LA TANZANIA

# Jarida la BUNGE

ISSN-085-6046 TOLEO LA KUMI JUNI, 2025



# "Safari Ya Miaka Mitano Ya Bunge La 12"


Ilikuwa ni safari ambayo Bunge liliweza kutimiza majukumu yake ipasavyo


## Yaliyomo




Tuzo Maalum ya Bunge kwa Mhe. Rais UK 08






Bajeti Kuu ya Serikali 2025-26 UK 14

Dhana ya Kuvunjwa Kwa Bunge UK 12

Marekebisho ya Kanuni za Bunge UK 41


*Scan hii Code kusoma na kupakua jarida hili*

# Dibaji



Ndugu Msomaji,

Nakukaribisha kwenye Jarida la Bunge Toleo la Kumi, Toleo hili ni la mwisho kwa Bunge la 12 ambalo linafikia ukomo wake mwaka huu wa 2025.

Jarida hili pamoja na mambo mengine lina makala ambayo imechambua kwa kina safari ya miaka mitano ya Bunge la 12, tangu Bunge hilo lilipoanza Novemba, 2020 hadi Juni, 2025.

Sambamba na hilo kuna makala ambayo imechambua kuhusu dhana ya kuvunjwa kwa Bunge.

Pia Jarida hili lina habari kuhusu Tuzo Maalum ya Heshima ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipewa wakati wa hafla iliyofanyika katika Viwanja vya Bunge tarehe 31 Mei, 2025.

Aidha, habari nyingine ambazo zimeandikwa katika Jarida hili ni kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26, marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 pamoja na Kikao cha 19 cha Maspika wa Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Bunge la Afrika Mashariki kilichofanyika Jijini Dar es Salaam.

Mbali na hayo, Jarida hili lina makala ambazo ni mwendelezo wa uchambuzi kuhusu misingi ya utaratibu wa uendeshaji wa Bunge, usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma pamoja na umuhimu wa Kamati za Bunge.

Vilevile Jarida hili lina makala ambazo zimechambua kuhusu usikilizaji na upokeaji wa maoni ya umma katika mchakato wa kibunge na mchakato wa Utungaji Sheria.

Nawatakia usomaji mwema wa Jarida la Bunge.

Ndugu Baraka Leonard
Katibu wa Bunge.

**BODI YA UHARIRI**

**MLEZI WA JARIDA**
Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb)
Spika wa Bunge

**BODI YA UHARIRI**
Mwenyekiti
Ndg. Baraka Leonard

Makamu Mwenyekiti
Ndg. Zuhura Mtatifikolo

**WAJUMBE**
Ndg. Athuman Hussein, *ndc*
Ndg. Hanifa Masaninga
Ndg. Abdallah Hancha
Ndg. Chacha Nyakega

**WAHARIRI**
Mhariri
Ndg. Lawrence Raphaely

Mhariri Msaidizi
Ndg. Debora Sanja

**Limeandaliwa na:**
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA.
Nukushi: +255 26234218
Simu: +255 26 232276-5
Barua Pepe: cna@bunge.go.tz

*Scan hii Code kusoma na kupakua jarida hili*

# Yaliyomo


**Safari ya Miaka Mitano ya Bunge la 12** UK 02


**Bunge lampa Tuzo ya Heshima Rais Samia** UK 08


**Utaratibu wa Rais wa Kulivunja Bunge** UK 12


**Bajeti ya Utu na Kazi** UK 14


**Dkt. Tulia - Tuimarishe Mshikamano wa Jumuiya ya A.Mashariki kupitia matumizi ya teknolojia** UK 18



**Usikilizaji na Upokeaji wa Maoni ya Umma katika Mchakato wa Kibunge** UK 22


**Mchakato wa Kutunga Sheria Katika Bunge** UK 26


**Umuhimu wa Kamati za Bunge Katika Utekelezaji wa Madaraka ya Bunge** UK 29


**Makatibu wa Jumuiya ya A. Mashariki wanawajibu wa kufanikisha Jumuiya isiyo na mipaka** UK 33


**Usimamizi wa Kibunge wa Fedha za Umma** UK 36


**Bunge la 12 larekebisha Kanuni za Kudumu za Bunge** UK 41


**Misingi ya Utaratibu na Uendeshaji wa Bunge** UK 44


**Bunge lapitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025** UK 47



**Bunge Marathon Msimu wa Pili yavunja Rekodi** UK 50

# Safari ya Miaka Mitano ya Bunge la 12




Spika wa Bunge, Mhe. Dkt. **Tulia Ackson** akiongoza Kikao cha Bunge

Na. **Lawrence Raphaely**

Safari ya miaka mitano ya Bunge la 12 ilianza tarehe 13 Novemba, 2020 siku ambayo Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Magufuli alilifungua rasmi. Kufuatia kifo cha Rais wa Awamu ya Tano na Rais Samia Suluhu Hassan kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 22 Aprili, 2021 alilihutubia Bunge na kutoa mwelekeo wa uongozi wake.

Bunge la 12 linatarajiwa kufikia ukomo wake mwishoni mwa Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge tarehe 27 Juni, 2025 siku ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan atalihutubia na kulifunga.

Katika kipindi cha miaka mitano, yapo mambo mengi ambayo Bunge la 12 limetimiza, ikiwa ni pamoja na kukamilisha kikamilifu majukumu yake ya msingi ambayo ni kutunga Sheria, kuisimamia na kuishauri Serikali pamoja na kupokea, kujadili na kupitisha mipango mbalimbali ya Serikali. Mbali na hayo, zipo pia changamoto kadhaa ambazo zilijitokeza wakati wa uhai wa Bunge hilo ikiwemo mabadiliko ya kiuongozi na ya Wabunge waliofariki dunia. Hivyo makala hii itaangazia masuala hayo pamoja na mambo mengine ambayo yanalihusu Bunge la 12 katika uhai wake wa miaka mitano.

## Mabadiliko ya Kiuongozi

Miongoni mwa mabadiliko makubwa ya uongozi wakati wa uhai wa Bunge la 12 ni mabadiliko ya Spika wa Bunge ambapo Bunge la 12 lilianza chini ya uongozi wa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Ndugai ambaye alijiuzulu Januari 6, 2022 na badala yake Bunge lilimchagua Mheshimiwa Dkt.Tulia Ackson kuwa Spika wa Bunge kuanzia Februari 1, 2022 hadi sasa.

Aidha, kufuatia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Mussa Zungu alichaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge tarehe 04 Oktoba, 2022 hadi sasa.

Kwa upande wa Katibu wa Bunge ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Bunge anayesimamia uratibu wa shughuli zote. Bunge la 12 limepita mikononi mwa Makatibu watatu wa Bunge, ambapo lilianza na Ndugu Stephen Kagaigai (2017-2021), Jaji Nenelwa Mwihambi (2021-2024) na Ndugu Baraka Leonard (2024 hadi sasa).

## Tume ya Utumishi wa Bunge

Sheria ya Uendeshaji Bunge imeweka msingi wa kuwepo kwa Tume ya Utumishi wa Bunge kwa lengo la uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge. Kifungu cha 12 cha Sheria hiyo kimeainisha Wajumbe watakaounda Tume hiyo ambapo




**Kanuni ya 7 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 inaanisha kwamba katika kuongoza Bunge, kutakuwa na Wenyeviti watatu wa Bunge ambao wataongoza vikao vya Bunge kwa utaratibu na maelekezo ya Spika au Naibu Spika kwa mujibu wa Kanuni**

viongozi watano ambao ni Spika wa Bunge, Naibu Spika wa Bunge, Waziri anayehusika na masuala ya Sera, Bunge, na Uratibu na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni wanakuwa Wajumbe wa Tume hiyo kwa nafasi zao.

Wajumbe wengine wa Tume hiyo ni Wabunge saba ambao wanachaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge wanaounda Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miongoni mwa Wajumbe hao saba, watano wanatokana na Chama Tawala na wawili wanatokana na Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni na Katibu wa Bunge anakuwa Katibu wa Tume.

Hadi Bunge la 12 linafikia ukomo wake Wajumbe wa Tume hiyo ni; Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson-Mwenyekiti wa Tume, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu-Makamu Mwenyekiti wa Tume, Mheshimiwa William Lukuvi-Mjumbe, Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hillaly -Mjumbe, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi-Mjumbe, Mheshimiwa Janejelly James Ntate-Mjumbe, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji-Mjumbe, Mheshimiwa Fakharia Shomar - Mjumbe, Khamis, Mheshimiwa Halima James Mdee-Mjumbe, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa - Mjumbe na Ndg. Baraka Leonard-Katibu wa Tume.



Wenyeviti wa Bunge, Mhe. **Deodatus Mwanyika** na Mhe. **Najma Murtaza Giga** wakiongoza ikao vya Bunge kwa nyakati tofauti



Waziri Mkuu, Mhe. **Kassim Majaliwa** akijibu Maswali Bungeni

### Wenyeviti wa Bunge

Kanuni ya 7 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 inaainisha kwamba katika kuongoza Bunge, kutakuwa na Wenyeviti watatu wa Bunge ambao wataongoza vikao vya Bunge kwa utaratibu na maelekezo ya Spika au Naibu Spika kwa mujibu wa Kanuni. Hadi Bunge hili la 12 linafikia ukomo Waheshimiwa Wabunge ambao kwa sasa wanahudumu katika nafasi hiyo ni pamoja na; Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mwenyekiti Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria); Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mwenyekiti Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo) na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii).

### Mchanganuo wa Wabunge

Bunge la 12 lina jumla ya Wabunge 393 ambapo; miongoni mwao Wabunge 364 ni wa Chama Tawala (Chama Cha Mapinduzi) na Wabunge 29 ni wa Kambi ya Walio Wachache Bungeni. Miongoni wa mwa Wabunge hao, Wabunge 264 walichaguliwa kuwakilisha majimbo ya uchaguzi, Wabunge watano walitoka katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Wabunge 113 wa Viti Maalam, Wabunge 10 wa Kuteuliwa na Rais na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye anaingia Bungeni kwa nafasi yake.

### Maswali

Katika kipindi cha miaka mitano ya Bunge la Kumi na Mbili na hadi kufikia Juni 20, 2025 jumla ya Maswali ya msingi ya kawaida 5,204 na zaidi ya 16,000 maswali ya Nyongeza yaliulizwa na Wabunge na kujibiwa na Serikali. Aidha, maswali 220 yaliulizwa na kujibiwa na Waziri Mkuu chini ya Kanuni ya 44 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari,2023.

### Miswada na Sheria

Bunge la 12 kwa kipindi cha miaka mitano katika kutekeleza jukumu lake mama la kutunga sheria, lilijadili na kupitisha miswada



Naibu Spika wa Bunge, Mhe. **Mussa Azzan Zungu** akiongoza Kikao cha Bunge

> Bunge la 12 lilifanikisha pia uteuzi za **Hayati Dkt. Faustine Ndugulile** kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, ambapo baada ya kifo chake **Dkt. Mohamed Janab**i alifanikiwa kuchukua nafasi yake.

takribani 59 ambayo hatimaye ilipata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Miongoni mwa miswada hiyo ambayo ilipitishwa na Bunge na hatimaye kupata kibali cha Mheshimiwa Rais ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2021, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu wa Mwaka 2022.

Miswada mingine ni Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2022, Muswada wa Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2023, Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024.

### Maazimio

Kwa upande wa Maazimio, Bunge la 12 kwa muda wa miaka mitano liliridhia Maazimio takribani 16 ambayo yaliwasilishwa na Serikali na Waheshimiwa Wabunge Bungeni.

Miongoni mwa Maazimio hayo ni Azimio la Bunge lililotokana na Hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Zainab Athman Katimba kuhusu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa miongoni mwa viongozi wenye ushawishi mkubwa duniani na kupewa Tuzo ya Babacar Ndiayo kwa Mafanikio ya Ujenzi wa Miundombinu ya ujenzi hususan barabara. Azimio hili liliridhiwa na Bunge tarehe 26 Mei, 2022 wakati wa Mkutano wa saba wa Bunge la 12.

Azimio lingine ambalo liliridhiwa na Bunge la 12 wakati wa Mkutano wa 11 ni Azimio kuhusu Pendekezo la Kuridhiwa Makubaliano Baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kwa lengo la Kuanzisha Ushirikiano wa Kiuchumi na Kijamii katika Uendeshaji wa Maeneo ya Bandari Nchini. Kuridhiwa kwa Azimio hilo kumesaidia kwa kiasi kikubwa kuleta mageuzi katika ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam na kuongeza mapato ya serikali.

> **Bunge la 12 kwa kipindi cha miaka mitano lilipokea, likajadili na kupitisha jumla ya hoja nne binafsi za Waheshimiwa Wabunge. Hoja hizo ni pamoja na maazimio mawili ya Bunge ambayo yalitokana na hoja binafsi za Waheshimiwa Wabunge.**

### Hoja Binafsi za Waheshimiwa Wabunge

Bunge la 12 kwa kipindi cha miaka mitano lilipokea, likajadili na kupitisha jumla ya hoja nne binafsi za Waheshimiwa Wabunge. Hoja hizo ni pamoja na maazimio mawili ya Bunge ambayo yalitokana na hoja binafsi za Waheshimiwa Wabunge.

Hoja ya kwanza ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga wakati wa Mkutano wa Tatu na baadaye kuwa Azimio la Bunge ilikuwa kuhusu Bunge kuutambua na kuuenzi mchango wa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa utumishi wake uliotukuka.

Hoja ya pili ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama pia wakati wa Mkutano wa Tatu na baadaye kuwa Azimio la Bunge ilikuwa kuhusu Bunge kumpongeza



Mwenyekiti wa Bunge, Mhe. **Dkt. Kizito Mhagama** akiongoza Kikao cha Bunge

> **Safari ya miaka mitano ya Bunge la 12 haikuwa tambarare na shwari muda wote, kuna wakati masikitiko na simanzi vililikumba Bunge hilo baada ya kuondokewa na wapedwa wake**





Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hoja nyingine binafsi ambayo Bunge liliipokea, kuijadili na kuipitisha ni hoja kuhusu kuwahamishia Maafisa Ushirika katika Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Maafisa Ugani chini ya Wizara ya Kilimo. Hoja hiyo iliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa 13 wa Bunge na Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole.

Bunge la 12 pia liliipokea, kuijadili na kuipitisha hoja nyingine binafsi kuhusu Halmashauri za Miji na Wilaya kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika kutatua tatizo la upungufu wa magari ya zimamoto pamoja na vifaa vinavyotumika kuzima moto na uokoaji. Hoja hiyo iliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa 15 wa Bunge na Mbunge wa Moshi Mjini, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo.

### Uwakilishi wa Bunge Kimataifa

Katika Medani za Kimataifa, Bunge la 12 limefanikiwa kung'ara

> **Bunge lilifanikiwa kuchukua nafasi ya juu kabisa ya uongozi wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) kufuatia Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja huo katika uchaguzi uliofanyika tarehe 27 Oktoba, 2023 Jijini Luanda, Angola. Mheshimiwa Dkt. Tulia ni mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika kushika nafasi hiyo.**

na kuandika historia ya kipekee. Kwa kuanza Bunge liling'ara kwa kuwasimamisha wagombea na hivyo kushika nafasi mbalimbali katika ngazi za kimataifa kwenye vyama vya kibunge.

Bunge lilifanikiwa kuchukua nafasi ya juu kabisa ya uongozi wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) kufuatia Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja huo katika uchaguzi uliofanyika tarehe 27 Oktoba, 2023 Jijini Luanda, Angola. Mheshimiwa Dkt. Tulia ni mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika kushika nafasi hiyo.

Aidha, Bunge la 12 lilifanikisha pia uteuzi za Hayati Dkt. Faustine Ndugulile kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, ambapo baada ya kifo chake Dkt. Mohamed Janabi alifanikiwa kuchukua nafasi yake.

Bunge pia limekuwa na mchango mkubwa katika uteuzi wa Dkt. Deo Mwapinga kuwa Katibu Mkuu wa Jukwaa la Mabunge ya Nchi Wanachama wa Ukanda wa Maziwa Makuu.

Mbali na hayo Bunge la 12 katika nyanja ya kimataifa limekuwa pia na ushiriki mzuri katika vyombo vya kibunge vya kikanda na kimataifa. Miongoni na vyombo hivyo ambavyo Bunge la 12 limekuwa na uwakilishi ni; Chama cha Mabunge ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola-Kanda ya Afrika, Umoja

**Katika kipindi cha miaka mitano cha Bunge la 12 Wajumbe tisa (9) ambao walichaguliwa na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kuiwakilisha Nchi katika Bunge la Afrika Mashariki ni pamoja na; Mheshimiwa Angela Charles Kizigha, Mheshimiwa Nadra Juma Mohamed, Mheshimiwa Dkt. Gladness Ladislaus Salema ambaye alichukuwa nafasi ya Hayati Dkt. Shogo Richard Mlozi, Mheshimiwa Dkt. Abdulla Hasnuu Makame, Mheshimiwa Machano Ali Machano, Mheshimiwa Mashaka Khalfan Ngole, Mheshimiwa Ansar Abubakar Kachwamba, Mheshimiwa James Kinyasi Millya na Mheshimiwa Dkt. Ng'waru Jumanne Maghembe.**

wa Mabunge Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC PF), Bunge la Afrika (PAP), Umoja wa Mabunge ya Afrika, Carribean Pasifiki na Jumuiya ya Ulaya (OACP/EU), Jukwaa la Kibunge la Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola, Umoja wa Kamati za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma katika Umoja wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCO-PAC)

Kwa upande mwingine Bunge la 12 pia lilikuwa mwenyeji wa mikutano kadhaa ambayo ilichangia kuitangaza Tanzania kimataifa. Mikutano hiyo ni pamoja Mkutano wa 53 wa Chama cha Mabunge ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola-Kanda ya Afrika, Mkutano wa 53 wa mwaka wa Jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC-PF) iliyofanyika Arusha. Mkutano mwingine ni Mkutano wa 19 wa Jukwaa la Maspika wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Dar es Salaam.

### Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA)

Katika kipindi cha miaka mitano cha Bunge la 12 Wajumbe tisa (9) ambao walichaguliwa na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kuiwakilisha nchi katika Bunge la Afrika Mashariki ni pamoja na; Mheshimiwa Angela Charles Kizigha, Mheshimiwa Nadra Juma Mohamed, Mheshimiwa Dkt. Gladness Ladislaus Salema ambaye alichukuwa nafasi ya Hayati Dkt. Shogo Richard Mlozi, Mheshimiwa Dkt. Abdulla Hasnuu Makame, Mheshimiwa Machano Ali Machano, Mheshimiwa Mashaka Khalfan Ngole, Mheshimiwa Ansar Abubakar Kachwamba, Mheshimiwa James Kinyasi Millya na Mheshimiwa Dkt. Ng'waru Jumanne Maghembe.

### Wabunge Waliofariki

Safari ya miaka mitano ya Bunge la 12 haikuwa tambarare na shwari muda wote, kuna wakati masikitiko na simamizi vililikumba Bunge hilo baada ya kuondokewa na wapedwa wake.

Huzuni ilitanda katika anga lote la Bunge la Tanzania, Waheshimiwa Wabunge walipomuaga Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati John Magufuli tarehe 22 Machi, 2021 katika viwanja vya Bunge Jijini Dodoma.

Aidha, katika kipindi cha miaka mitano cha Bunge la 12, Wabunge tisa (9) wafariki. Waheshimiwa Wabunge hao waliofariki ni pamoja na Martha Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Injinia Atashasta Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Muhambwe, Khatib Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Konde na Elias Kwandikwa aliyekuwa Mbunge wa Ushetu.

Wengine ni William Olenasha aliyekuwa Mbunge wa Ngorongoro, Irene Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Francis Mtenga aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali na Dkt. Faustine Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni.

Mbali na Wabunge hao ambao walipoteza maisha, wapo ambao walikoma kuwa Wabunge kwa sababu nyinginezo. Waheshimiwa hao ni pamoja na Mheshimiwa Prof. Balozi Adelardus Lubango Kilangi, Mheshimiwa Balozi Humphrey Polepole na Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk. Wabunge hao wote watatu walikoma kuwa Wabunge baada ya kuteuliwa kuwa Mabalozi na Mheshimiwa Rais katika vipindi tofauti. Aidha Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi alikoma kuwa Mbunge baada ya kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.

### Hitimisho

Kufikia hapo tumeona kwamba safari ya miaka mitano ya Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa ni safari iliyobeba mijadala mikubwa ya kitaifa, ufanisi wa Bunge katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo ya kutunga sheria, kusimamia na kuishauri Serikali pamoja na kuwakilisha wananchi. Na ni wazi kuwa Bunge la 12 limekua sehemu muhimu ya mabadiliko na maendeleo ya nchi katika kipindi hiki na katika kutekeleza majukumu yake.Bunge hilo limekuwa pia na ushirikiano mkubwa na Serikali hususani katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti na miradi ya kimkakati.

# Haya ndiyo yaliyosukuma Bunge kumpa Tuzo ya Heshima Rais Samia

Na **Zuhura Mtatifikolo**

**Mei 31, 2025, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliandika historia mpya kwa kumtunuku Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Tuzo Maalum ya Heshima kutokana na mchango wake katika kuleta maendeleo kwa Watanzania na kuimarisha misingi ya utawala bora.**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. **Samia Suluhu Hassan** akipokea Tuzo Maalum ya Heshima ya Bunge la Tanzania, kutoka kwa Spika wa Bunge hilo, Mhe. **Dkt. Tulia Ackson**

Tuzo hiyo ilitolewa kwa heshima ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake tangu achukue madaraka mwaka 2021.

Katika hafla hiyo iliyofanyika kwenye viwanja vya Bunge Dodoma, Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, aliainisha mafanikio makubwa yaliyowezesha uamuzi wa Bunge la 12 kumtunuku Tuzo Rais Samia.

Kwa mujibu wa Spika Tulia, uongozi wa Rais Samia umejikita katika misingi ya uwajibikaji, uwazi, haki za binadamu, usawa na ujumuishi, vigezo vinavyobeba dhana ya utawala bora.

"Tunajivunia uongozi wako wa miaka minne ambao umeakisi utawala bora, weledi, uwajibikaji, uaminifu na ujumuishi. Umekuwa kiongozi wa mfano katika kuimarisha mifumo ya sheria, haki za binadamu, na uwazi unaozingatia usawa na maendeleo ya kila mwananchi.

"Kwa nafasi yetu Wabunge, tumeshuhudia historia ya mafanikio na mabadiliko yaliyoleta tija na ustawi kwa jamii nzima,"anasema.

Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka **Dar es Salaam hadi Makutupora (km 722**) umefikia hatua nzuri. **Serikali imenunua vichwa 17 vya treni na mabehewa 65.** Ujenzi wa vipande vya Mwanza-Isaka, Makutupora-Tabora na Tabora-Kigoma unaendelea.

Spika wa Bunge, Mhe. Dkt. Tulia Ackson

### Dira ya R-Nne: Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Kujenga Upya

Mojawapo ya mafanikio makubwa ya Rais Samia ni uanzishaji wa falsafa ya R-Nne (Reconciliation, Reforms, Resilience na Rebuilding), ambayo imesheheni maono ya maridhiano ya kisiasa na kijamii, mageuzi ya kiutendaji, uimara wa taasisi na ujenzi mpya wa taifa katika misingi ya mshikamano.

Kwa mujibu wa Spika Tulia, kupitia dira hii, Rais Samia ameweza kukuza Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa kuhakikisha wananchi wanashiriki na kunufaika kwa usawa. Takriban hoja 15 za Muungano zimepatiwa ufumbuzi, hali inayoonyesha dhamira ya kweli ya kuimarisha ushirikiano wa pande mbili za Muungano.

"Tanzania ni nchi yenye amani, utulivu, umoja na mshikamano ambavyo ndivyo nguzo za kudumisha Muungano wa Tanzania Bara na Zanzibar na kuwawezesha wananchi wa Tanzania kufurahia matunda ya Muungano huu kwa kudumisha utaifa wetu uliojengwa katika misingi ya jamii mbili zenye udugu wa asili," anasema.

Anasema Bunge la Tanzania limeendelea kufarijika kuona Serikali ya Awamu ya Sita ikiendelea kuulinda, kuuthamini na kuudumisha Muungano.

### Sekta ya Elimu: Ongezeko la Bajeti, Miundombinu na Udahili

Spika Tulia alisema Serikali imefanya upanuzi mkubwa wa miundombinu ya elimu sambamba na kuongeza bajeti ya elimu ya juu na kutoa mikopo kwa wanafunzi wa stashahada katika fani za sayansi, afya na ufundi. Mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 yamezaa Sera mpya ya Elimu ya mwaka 2023 inayosisitiza matumizi ya teknolojia na mafunzo ya amali.

"Fedha kwa ajili ya mpango wa Elimu Bila Ada zimeongezeka kutoka Sh. bilioni 312.5 mwaka 2020 hadi Sh. bilioni 796.38 mwaka 2024. Udahili wa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi umeongezeka kutoka 344,815 hadi 440,000 huku udahili wa elimu ya juu ukiongezeka kutoka 98,003 mwaka 2020 hadi 196,837 mwaka 2023. Serikali pia imeajiri walimu 89,778," alisema

Kwa shule za msingi, anasema idadi imeongezeka kutoka shule 16,656 mwaka 2020 hadi shule 19,783 mwaka 2024, na shule za sekondari kutoka 5,001 hadi 5,926 katika kipindi hicho hicho.

### Sekta ya Madini: Mapato Yaongezeka

Anasema Serikali imefanikiwa kuongeza mapato kutoka Sekta ya Madini kutoka Sh. bilioni 624.61 mwaka 2021 hadi bilioni 753.82 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 20.7. Vituo vya ununuzi wa madini vimeongezeka kutoka 40 hadi 105, na mitambo mitano ya uchorongaji imenunuliwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Mitambo minne ya kuzalisha mkaa mbadala pia imenunuliwa kwa gharama ya Sh. bilioni 12.86.

### Sekta ya Utalii: Watalii Waongezeka

Dkt.Tulia anasema mapato ya Serikali kutoka sekta ya utalii yameongezeka kutoka Sh. bilioni 367 mwaka 2020 hadi bilioni 877 Machi 2025, ongezeko la asilimia 120. Idadi ya watalii wa kimataifa imepanda kutoka 620,867 mwaka 2020 hadi 2,141,895 mwaka 2024.

"Filamu za The Royal Tour na Amazing Tanzania zimechangia kuitangaza Tanzania kimataifa. Mapato ya utalii wa ndani yamepanda kutoka Sh. bilioni 46.3 mwaka 2021 hadi bilioni 209.8 mwaka 2024. Tanzania pia imetunukiwa tuzo mbalimbali za kimataifa, ikiwemo Africa's Leading Destination 2024 na World's Leading Safari Destination 2024,"anasema.

### Sekta ya Kilimo: Mabwawa, Skimu na Mbolea zaongeza ufanisi

Mheshimiwa Spika anaeleza kilimo cha umwagiliaji kimeongezwa kutoka hekta 561,383 hadi hekta 983,466 mwaka 2024 na kwamba Serikali imejenga mabwawa 19 ya uvunaji wa maji na skimu za umwagiliaji 34. Aidha, upatikanaji wa mbolea umeongezeka kutoka tani 586,604 mwaka 2020 hadi tani 1,213,729.

"Viwanda vipya 18 vya ushirika vimejengwa na idadi ya vyama vya ushirika vinavyotumia mfumo wa stakabadhi za ghalani imeongezeka kutoka 2,150 hadi 4,060. Vyama vipya 49 vimeanzishwa kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu,"alisema.

Mapato ya Serikali kutoka **sekta ya utalii yameongezeka kutoka Sh. bilioni 367 mwaka 2020 hadi bilioni 877 Machi 2025,** ongezeko la asilimia 120. **Idadi ya watalii wa kimataifa imepanda kutoka 620,867 mwaka 2020 hadi 2,141,895 mwaka 2024. -** *Dkt.Tulia*

> Kwa niaba ya CCM na wananchi wapenda maendeleo na amani nchini tunamhakikishia Rais ushirikiano wa dhati, mshikamano usiotekeleka na uungaji mkono mkubwa muda wote anapotimiza wajibu wake kwa watanzania wote



### Sekta ya Afya: Vifo vya Mama na Mtoto vyashuka

Alisema vifo vya mama wakati wa kujifungua vimepungua kutoka 556 mwaka 2016 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2025.

Alieleza kuwa hatua hiyo inatokana na Serikali kujenga hospitali za kanda sita, hospitali za rufaa za mikoa 28, hospitali za wilaya 129, vituo vya afya 345 na zahanati 1,158.

"Kwa mafanikio haya, Rais ametunukiwa Tuzo ya Kimataifa ya "The Global Goalkeeper Award" na taasisi ya Gates Foundation,"alisema.

### Sekta ya Maji: Tanzania yapiga hatua kubwa

Kupitia kaulimbiu ya Kumtua Mama Ndoo Kichwani, anasema Serikali imefanikiwa kusambaza maji katika vijiji zaidi ya 10,000, huku visima 900 vikichimbwa kote nchini. Ujenzi wa Gridi ya Maji ya Taifa umeanza, na Tanzania imeongoza Ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini kwa kuanzisha hatifungani ya kijani ya maji.

Anasema miradi mikubwa ya Kidunda (sh.bilioni 329.5) na Farkwa (sh.bilioni 312) imeanza kutekelezwa. Serikali imenunua seti 25 za mitambo ya kuchimba visima na seti tano za kuchimba mabwawa.

### Sekta ya Ujenzi: Miundombinu ya Barabara na Madaraja yaimarishwa

Alisema barabara za lami zimeongezeka kutoka kilomita 13,235.1 mwaka 2020 hadi 15,336.36 mwaka 2024. Barabara za changarawe zimeongezeka kutoka kilomita 29,133 hadi 42,059.17. Viwanja vya ndege vya mikoa mbalimbali vimekarabatiwa na ujenzi wa Uwanja wa Kimataifa wa Msalato umefikia asilimia 64.

Pia, alisema madaraja makubwa kama Kigongo-Busisi, Tanzanite na Wami yamekamilika.

### Sekta ya Uchukuzi: Reli, Bandari na Ndege zapiga hatua

Anasema ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora (km 722) umefikia hatua nzuri. Serikali imenunua vichwa 17 vya treni na mabehewa 65. Ujenzi wa vipande vya Mwanza-Isaka, Makutupora-Tabora na Tabora-Kigoma unaendelea.

Kiongozi huyo alisema Bandari za Dar es Salaam na Tanga zimeboreshwa, zikiwemo gati, kina na uwezo wa kuhudumia shehena kubwa. Shehena ya mizigo imeongezeka kutoka tani milioni 17.1 hadi 28.75 mwaka 2024.

Katika usafiri wa anga, alisema serikali imenunua ndege saba mpya na sasa ATCL inamiliki ndege 16, kutoka ndege tisa mwaka 2020.



> **Tuzo ya heshima iliyotolewa na Bunge kwa Rais Samia ni uthibitisho kuwa uongozi wake umetafsiri matarajio ya Watanzania kwa vitendo. Kutoka utulivu wa kisiasa, ustawi wa kijamii hadi ukuaji wa uchumi, safari ya miaka minne imekuwa ya mabadiliko makubwa na ya kutia moyo.**

### Alichosema Rais Samia na safari yake ya uongozi

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Rais Samia anagusia mazingira magumu aliyoyakuta alipokabidhiwa ofisi ya urais mwaka 2021.

Alikumbuka kuwa wakati huo Taifa lilikuwa linapitia mshtuko mkubwa kutokana na kifo cha Rais Dkt. John Magufuli, changamoto za kiuchumi na hofu ya ugonjwa wa Covid-19.

"Wakati huo mazingira ya kisiasa, kijamii na kiuchumi hayakuwa rafiki, lakini nilimwomba Mungu anijalie hekima kama ya Nabii Suleiman na kuniongoza kama alivyowaongoza manabii wake," anasema Rais Samia.

Anasema mafanikio yaliyotambuliwa na Bunge si ya kwake binafsi, bali ni ya wananchi wote, wabunge, na watumishi waliotekeleza majukumu yao kwa weledi na uzalendo. "Tuzo hii si yangu pekee, ni ya Watanzania wote," alisema.

Rais Samia anatoa shukrani kwa Bunge kwa kuonesha ushirikiano, kuchambua bajeti kwa kina, na kuisimamia Serikali kwa njia ya hoja zenye mashiko. Aliwataka wabunge kuendelea kuweka mbele maslahi ya taifa na wananchi.

Tuzo ya heshima iliyotolewa na Bunge kwa Rais Samia ni uthibitisho kuwa uongozi wake umetafsiri matarajio ya Watanzania kwa vitendo. Kutoka utulivu wa kisiasa, ustawi wa kijamii hadi ukuaji wa uchumi, safari ya miaka minne imekuwa ya mabadiliko makubwa na ya kutia moyo.

Rais Samia anaweka wazi kuwa mafanikio hayo ni matokeo ya imani, maombi, mipango madhubuti, na kazi ya pamoja

"Mamlaka yote huwekwa na Mwenyezi Mungu. Ninamshukuru kwa nafasi hii na ninaipokea tuzo hii kwa niaba ya Watanzania wote." alishukuru Mheshimiwa Rais.

### CCM yapongeza

Chama cha Mapinduzi (CCM) kinatoa pongezi kwa Mwenyekiti wa CCM na Rais Samia Suluhu Hassan kwa heshima kubwa aliyopewa na Bunge ya kutunukiwa Tuzo Maalum ya Heshima.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, anasema Tuzo hiyo ni kielelezo kingine cha kuthibitisha mchango mkubwa wa kipekee wenye matokeo chanya wa kazi nzuri zilizofanywa na Rais Samia katika kulijenga Taifa.

Anasema Tuzo hiyo ni ushindi wa wazi wa kuthaminiwa kwa uongozi madhubuti wa Rais Samia unaojengwa juu ya misingi ya amani, maridhiano ya kisiasa, mshikamano wa kitaifa na maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi kwa watanzania wote.

"Ni matokeo ya utekelezaji wenye mafanikio makubwa wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM chini ya Serikali ya Awamu ya Sita. Aidha, tunajivunia kuwa Rais Samia anayendelea kuthibitisha uimara, umakini na weledi wa chama katika kutoa uongozi thabiti kwa nchi yetu."

"Ni fahari kwa CCM kuwa na kiongozi mwenye maono, uthubutu na dira ya mandeleo jumuishi kwa wote."

"Kwa niaba ya CCM na wananchi wapenda maendeleo na amani nchini tunamhakikishia Rais ushirikiano wa dhati, mshikamano usiotetereka na uungaji mkono mkubwa muda wote anapotimiza wajibu wake kwa watanzania wote,"alisema.

Makalla anasema Tuzo hiyo inaungana na tuzo nyingi za heshima alizopokea Rais za ndani na nje ya nchi kama ishara ya kutambua mchango wake wa kipekee katika kuimarisha utawala bora, kuhimiza maendeleo shirikishi na kuendeleza taswira chanya ya Tanzania kimataifa.

"CCM ina imani kubwa na uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia katika kuliongoza Taifa kwa amani, ustawi na mafanikio ya kweli,"alisema.

# Utaratibu wa Rais wa Kulivunja Bunge



**Rais anayo mamlaka chini ya Katiba ya kuitisha Bunge jipya mara baada ya kuhitimishwa kwa Uchaguzi Mkuu kwa kutoa Tangazo katika Gazeti la Serikali. Kupitia Tangazo hilo Rais atataja tarehe rasmi ya Bunge jipya kukutana.**

Na **Deborah Sanja**

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Ibara ya 62 (1) na (2) inaeleza kwamba kutakuwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambalo litakuwa na sehemu mbili, yaani Rais na Wabunge.

Ibara ya 63 (2) ya Katiba inaeleza kwamba, Bunge ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake.

Katika kutekeleza majukumu na madaraka, Bunge linaweza kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake. Vilevile, Bunge linayo madaraka ya kujadili utekelezaji wa majukumu ya kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa Bajeti unaofanyika kila mwaka.

Vilevile Bunge linaweza kujadili na kuidhinisha Mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano. Mipango hiyo inalenga kuleta maendeleo kwa watu kupitia miradi mbalimbali pamoja na kukuza uchumi. Halikadhalika, Bunge linalo jukumu la kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.

Bunge pia linayo madaraka ya kutunga sheria pale ambapo linajitokeza jambo ambalo utekelezaji wake unahitaji usimamizi wa sheria pamoja na kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa na Bunge.

Hivyo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linafanya kazi ya kuisimamia na kuishauri Serikali, kuwakilisha maslahi ya wananchi Bungeni, kutunga sheria na kuridhia mikataba ya kimataifa.

Ibara ya 65 ya Katiba inaeleza kuhusu uhai wa Bunge. Ibara hiyo inaeleza kuwa muda wa uhai wa Bunge ni miaka mitano. Bunge la kwanza linahesabiwa kuwa lilianza mwaka 1965 ambapo ndipo uchaguzi wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulifanyika baada ya Tanganyika na Zanzibar

**Katiba imempa mamlaka Mheshimiwa Rais kuelekeza Spika na waliokuwa Wabunge mara kabla Bunge halijavunjwa wahudhurie Mkutano huo wa Bunge na wote watahesabiwa kuwa ndio Wajumbe wa Bunge kwa madhumuni ya Mkutano huo.**

kuungana. Tangu kipindi cha Bunge hilo la kwanza hadi sasa limefika–Bunge la 12 ambalo linatarajiwa kufika ukomo wake katikati ya mwaka huu wa 2025.

Kwa kawaida Bunge linapomaliza kipindi chake cha miaka mitano, kwa Mamlaka aliyopewa kikatiba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hulivunja Bunge ili kupisha Uchaguzi Mkuu kufanyika.

Ibara ya 65(2) ya Katiba inaeleza kwamba maisha ya Bunge ni kuanzia tarehe ambayo Bunge jipya limeitishwa kukutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu na huisha tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge ili kuwezesha Uchaguzi Mkuu wa kawaida kufanyika.

Rais anayo mamlaka chini ya Katiba ya kuitisha Bunge jipya mara baada ya kuhitimishwa kwa Uchaguzi Mkuu kwa kutoa Tangazo katika Gazeti la Serikali. Kupitia Tangazo hilo Rais atataja tarehe rasmi ya Bunge jipya kukutana.

Katika kikao cha kwanza cha Bunge jipya, shughuli ya kwanza inakuwa ni kusomwa kwa Tangazo la Mheshimiwa Rais linaloitisha Bunge. Baada ya Tangazo hilo kusomwa hufuata uchaguzi wa Spika. Mara baada ya kiongozi huyo kupatikana, shughuli yake ya kwanza huwa ni kusimamia kiapo cha uaminifu kwa Wabunge. Zoezi hilo linapokamilika hufuata Bunge kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu na kisha Uchaguzi wa Naibu Spika hufanyika. Baada ya shughuli hizo kumalizika ndipo Rais huja Bungeni kwa ajili ya ufunguzi rasmi ya Bunge jipya.

Kipindi kingine cha miaka mitano kinapopita, Rais hutumia mamlaka aliyopewa kikatiba ya kulivunja Bunge kwa kutoa Hati/Tangazo maalum katika Gazeti la Serikali ambalo hutaja tarehe na mwezi ambao analivunja Bunge hilo. Baada ya Tangazo hilo,Mheshimiwa Rais hupanga tarehe ya atakayofika Bungeni kutoa Hotuba ya kulifunga Bunge linalomaliza muda wake. Aidha, Mheshimiwa Rais anaweza kufika Bungeni kwa ajili ya kutoa hotuba ya kulifunga Bunge na baada ya hapo kutoa Tangazo katika Gazeti la Serikali la kulivunja Bunge.

Hivyo, utaratibu wa kisheria unaonesha kuwa, Rais anapofika Bungeni na kuhutubia, hutumia nafasi hiyo kulifunga Bunge na siyo kulivunja. Bunge huvunjwa kupitia Tangazo la Mheshimiwa Rais katika Gazeti la Serikali linaloeleza kuwa Bunge limevunjwa rasmi. Hivyo, Bunge huweza tu kuvunjwa kupitia Tangazo la kulivunja Bunge, linalotolewa na Mheshimiwa Rais katika Gazeti la Serikali.

Bunge linaloendelea kwa sasa linatarajia kumaliza muda wake mwaka huu ili kupisha Uchaguzi Mkuu kufanyika. Kwa ajili hiyo, ratiba ya Mkutano wa 19 wa Bunge inaonesha kuwa tarehe 27 Juni, 2025 Mheshimiwa Rais anatarajiwa kufika Bungeni kulihutubia na kisha kulifunga rasmi Bunge.

Kwa utaratibu huo na katika kipindi hicho Mheshimiwa Rais anatarajiwa kutoa Tangazo la Kuvunja Bunge katika Gazeti la Serikali katika siku na tarehe atakayoona inafaa.

Pamoja na Mheshimiwa Rais kuwa na mamlaka ya kikatiba ya kulivunja Bunge linapomaliza muda wa miaka mitano, Ibara ya 90 (2) ya Katiba imeainisha mazingira mengine ambayo Mheshimiwa Rais anaweza kulivunja Bunge.

Mazingira hayo ni pamoja na wakati Bunge linapokataa kupitisha Bajeti iliyopendekezwa na Serikali na endapo, kutokana na uwiano wa uwakilishi wa Vyama vya Siasa katika Bunge, Rais ataona kwamba hakuna uhalali wa Serikali iliyopo madarakani kuendelea kuwapo, na wala haupo uwezekano wa kuunda Serikali mpya.

Vilevile Rais anaweza kulivunja Bunge iwapo Bunge litakataa kupitisha hoja ambayo ni ya msingi katika sera za Serikali, na ikiwa ataona suluhisho lililopo si kuteua Waziri Mkuu mwingine bali ni kuitisha Uchaguzi Mkuu na Bunge. Sababu nyingine inayoweza kusababisha Bunge kuvunjwa ni inapotokea Bunge linakataa kupitisha Muswada wa Sheria kwa mujibu wa ibara ya 97(4) ya Katiba

Ibara ya 97 (4) inaeleza kwamba; Iwapo Muswada umerudishwa kwa Bunge na Rais, halafu ukaungwa mkono kwenye Bunge na Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote na kupelekwa kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake kwa mara ya pili kabla haujamalizika muda wa miezi sita tangu uliporudishwa, basi Rais atatakiwa kuukubali Muswada huo kabla ya kumalizika muda wa siku ishirini na moja tangu Muswada huo ulipowasilishwa kwake la sivyo basi itabidi alivunje Bunge.

Aidha, Katiba imempa mamlaka Mheshmiwa Rais kurefusha uhai wa Bunge au kuliitisha Bunge lililovunjwa katika mazingira ambayo atalazimika kufanya hivyo.

Ibara ya 90 (3) inaeleza kwamba muda wa maisha ya Bunge ukimalizika Bunge litahesabiwa kuwa limevunjwa isipokuwa kwamba muda huo ukiisha wakati wowote ambapo Jamhuri ya Muungano iko katika vita Bunge laweza mara kwa mara kuongeza muda usiozidi miezi kumi na kwamba maisha ya Bunge hayawezi kuongezwa kwa muda unaozidi miaka mitano.

Ibara ya 90(4) inafafanua kuwa, kukitokea hali ya hatari au kama kuna hali ya hatari ambayo Rais anaona inasababisha kuitisha Mkutano wa Bunge na iwapo wakati huo Bunge limevunjwa na matokeo ya kura zilizo nyingi za Uchaguzi Mkuu hayajatangazwa basi Rais aweza kutoa Taarifa Maalum ya kuitisha Mkutano wa Bunge.

Katiba imempa mamlaka Mheshimiwa Rais kuelekeza Spika na waliokuwa Wabunge kabla Bunge halijavunjwa wahudhurie Mkutano huo wa Bunge na wote watahesabiwa kuwa ndio Wajumbe wa Bunge kwa madhumuni ya Mkutano huo.

Spika huyo na Wabunge hao watahesabiwa hivyo mpaka usiku wa manane wa siku yatakapotangazwa matokeo ya kura zilizo nyingi za Uchaguzi Mkuu.



# Bajeti ya Utu na Kazi

> **Sh56.49 trilioni zinazotarajia kukusanywa na kutumiwa kwa mwaka wa fedha 2025/26 huku fedha nyingi zikitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na miradi ya kimkakati**

**Trilioni**
**56.49**

Zinazotarajia kukusanywa na kutumiwa kwa mwaka wa fedha **2025/26** huku fedha nyingi zikitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na miradi ya kimkakati.

**Trilioni**
**40.47**
*Kiasi cha Mapato ya ndani kinachokadiriwa kugharamia Bajeti*

**Trilioni**
**1.07**
*Misaada kutoka nje*

**Trilioni**
**14.95**
*Mkopo*




Na. **Deonisius Simba**

Ni Bajeti ya Utu na Kazi, ni Bajeti ya Mkakati, ni Bajeti ya wananchi, ndivyo unavyoweza kusema ingawa wengine wanasema ni Bajeti ya matumaini inayowalenga wanyonge wa hali ya chini ili kuwainua.

Hii inatokana na wasilisho la Serikali kwa Wabunge siku ya Alhamisi ya Juni 12, 2025 wakati Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba alipokuwa akisoma Bajeti kuu ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026 ambayo ilionekana kujaa matumaini.

Bajeti hiyo yenye jumla ya Shilingi trilioni 56.49 zinazotarajiwa kukusanywa na kutumiwa kwa mwaka wa fedha 2025/26 huku fedha nyingi zikitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na miradi ya kimkakati.

Hii ni Bajeti ya nne kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndiyo Bajeti ya mwisho kwa Bunge la 12 kabla ya kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 2025.

Awali Serikali ilikusudia kuwa na Bajeti ya trilioni 57. 40 lakini ushauri wa Wabunge wakati wa michango kwenye Bajeti za Wizara, ilionekana wazi kuwepo na haja ya kufanya maboresho ambayo kwa sehemu kubwa yaliondoa utegemezi hasa katika mambo muhimu na ya msingi. Kiasi cha bilioni 550 kimepunguzwa kwenye makadirio ya awali hivyo fedha hizo zitapunguzwa kwenye baadhi ya miradi ya maendeleo ambayo ilitegemea zaidi fedha kutoka nje.

"Bajeti hii inatarajiwa kugharamiwa na mapato ya ndani ya trilioni 40.47, misaada kutoka nje trilioni 1.07 na mikopo ya trilioni 14.95," alisema Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na kulipua shangwe kutoka kwa Wabunge.

Ni wazi kuwa, kiasi cha fedha zinazotoka ndani ni kikubwa zaidi ukilinganisha na fedha zitakazopokelewa kutoka nje, hivyo ina onesha nia ya Serikali katika kujitegemea kwa asilimia kubwa. Moja ya sifa katika Bajeti ya 2025/2026 ni jinsi ilivyobeba vipaumbele ambavyo vinagusa moja kwa moja maisha ya Mtanzania wa hali ya chini ikiwemo kukamilisha utekelezaji wa miradi, programu za Maendeleo na afua zinazochangia maeneo makuu ya vipaumbele vya mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa.

Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uzalishaji wa bidhaa viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara na kuchochea maendeleo ya watu. Vingine ni kuendeleza rasilimali watu ili kuhakikisha ufikiwaji wa Dira ya Maendeleo ya 2025 na katika maeneo ya miradi ya kimkakati na ile ya kielelezo.

## Tumaini la Watanzania

Afya ni mtaji, maisha ya mwanadamu yanategemea uzima na uhai, katika Bajeti ya 2025/2026 Serikali imeweka mkakati wa kutafuta fedha kwa ajili ya kusaidia katika matibabu jambo linalotajwa kama ukombozi kwa Watanzania.

Wimbo wa muda mrefu wa Bima ya afya kwa wote umewekewa mkakati katika Bajeti hii na jambo hilo linakwenda kutekelezwa licha ya kuwa limechelewa lakini wahenga walinena 'kawia ufike'.

Hii si mara ya kwanza kwa Serikali kuanzisha vyanzo katika kuhudumia wananchi wake kwani ilishawahi kufanya hivyo kwenye maji na barabara na ikafanikiwa.

Ikiwa mkazo utawekwa, hapana shaka hofu juu ya kukosekana kwa dawa muhimu za kudhibiti maambukizi ya UKIMWI na safari ya mafanikio katika Bima ya Afya kwa wote itaanzia hapa na kuzaa matunda yaliyosubiriwa kwa muda mrefu.

Hofu iliyojengeka kutoka kwa baadhi ya watu kuhusu kuondolewa kwa misaada ya kudhibiti na kupambana na UKIMWI itakuwa imepungua kutoka miongoni mwa Watanzania.

## Kicheko kwa Wastaafu

Serikali imejibu kilio cha muda mrefu kutoka kwa Wabunge ambao wamekuwa wakipigania nyongeza ya pensheni kwa wastaafu wakitaka waboreshewe maisha yao kwa kuongezewa fedha.

Kwenye Bajeti ya 2025/2026 jambo hilo limepatiwa majibu kwani wataanza kunufaika na mpango wa nyongeza ya pensheni kuanzia Julai Mosi, 2025.

Bajeti inataja nyongeza hiyo imepanda kwa kima cha chini cha pensheni kwa wastaafu wanaolipwa na HAZINA kutoka Sh. 100,125.9 hadi kufikia Sh. 250,125.9 ambalo ni ongezeko la asilimia 149.8 kwa mkupuo.

Nyongeza hiyo ni ushindi kwa Wabunge kwani kipindi cha miaka mitano ya uhai wa Bunge hili, wamekuwa wakihoji kwa nini Serikali isiongeze kiwango cha pensheni ili kutoa unafuu kwa wastaafu ambao walitumikia Taifa kwa uaminifu.



**Mabadiliko ya kisera yanayoendelea duniani ambayo yaliyosababisha wadau muhimu wa maendeleo kupunguza misaada iliyokuwa inatolewa kwa ajili ya huduma za Afya hususani masuala ya UKIMWI, nalo limeangaziwa.**

**Hivi karibu Serikali ilijibu swali Bungeni ikieleza namna inavyoweka mkakati katika kukabiliana na changamoto hiyo ambayo imeikumba Dunia na katika kutimiza hilo, imeleta mwarobaini katika Bajeti.**

**"Serikali inapendekeza kuanzisha vyanzo vipya mbadala vya mapato ili kupunguza nakisi ya kibajeti kwa kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali ambapo asilimia 70 ya mapato yatakayoongezeka itapelekwa kwenye mfuko wa udhamini wa UKIMWI (ATF) na asilimia 30 itakwenda kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa wote," alisema Mheshimiwa Dkt. Mwigulu.**

**Kwa mujibu wa Serikali, fedha hizo zitapatikana kupitia vyanzo kama vinywaji vya kilevi vinavyoingizwa kutoka nje, ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano ya kielektroniki, mafuta, madini, kwenye zawadi za ushindi katika michezo ya kubahatisha na kutoza magari na mashine zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.**

**Ni wazi kuwa, vyanzo hivi na vingine vinaakisi malengo ya Serikali kwani vipo katika mzunguko wa kila siku kwenye maisha ya mwanadamu na muhimu katika kuwezesha uchumi na ulipaji wa kodi.**

Hata hivyo Serikali imeahidi kusimamia mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuhakikisha inabaki himilivu na kulipa mafao ya wastaafu wote kwa wakati kama sheria inavyosema.

### Makali bodaboda yaondolewa

Kundi kubwa la vijana wamejiajiri kupitia sekta ya usafirishaji ambapo wengi wanaendesha pikipiki za magurudumu mawili maarufu bodaboda na wengine wanatumia zile zenye magurudumu matatu ambazo ni bajaji na guta.

Tanzania ilirasimisha matumizi katika usafiri huu lakini umekuwa ukipigiwa kelele kutokana na faini zake kuangukia katika chombo cha moto ikiwemo leseni hivyo mwenye kosa la pikipiki uchukuliwa sawa na mwenye kosa wa basi la abiria. Kitendo hicho kimekuwa kikilalamikiwa na watunga sheria wakieleza mapungufu kwamba yanamuumiza mwendesha pikipiki.

Hata hivyo, katika Bajeti hii yenye matumaini makubwa ya wananchi, kilio cha bodaboda kimepata mtetezi na sasa wanakwenda kupata ahueni waliyoitamani muda mrefu.

Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Bajeti yake imepunguza ada ya usajili wa pikipiki za biashara kutoka Sh. 340,000 hadi Sh. 170,000 kwa miaka mitatu na ada hiyo italipwa wakati wa usajili pekee. Kingine ni ada ya leseni ya uendeshaji wa pikipiki, bajaji na guta kutoka Sh. 70,000 hadi Sh. 30,000 ambalo ni punguzo la kiwango kikubwa zaidi.

Kitendo hiki si kwamba kimepokelewa na kushangiliwa na waendeshaji tu, bali wawakilishi wa wananchi ambao ni Wabunge wamekuwa na nyuso za tabasamu na ushindi kwa kuwa wamefikisha kilio cha maofisa usafirishaji na kimepokelewa.

Kiwango kilichokuwa kinatozwa kilielezwa hakikuwa rafiki katika mazingira na hali za vijana wanaoendesha pikipiki wakidai kundi hili lilionewa hasa kwa kulinganisha na vyombo vingine vyenye uzito wa juu.

### Shabaha za Uchumi

Malengo ya Serikali katika Bajeti ya 2025/26 ni kuongeza kasi ya ukuaji wa pato halisi la Taifa hadi kufikia asilimia 6.0 kutoka ukuaji wa asilimia 5.5 mwaka uliopita.

Mpango wa kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei umeandaliwa ili kuhakikisha unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 hadi 5.0 katika muda wa kati na hili linawekewa msisitizo katika usimamizi wake. Ongezeko la mapato ya ndani kufikia asilimia 16.7 ya pato mwaka 2025/2026 yamechochea ari ya kuiamini Bajeti hii kwamba itakuwa na uhalisia katika utekelezaji ukilinganisha na asilimia 15.8 kwa Mwaka 2024/2025.

Hivyo, Serikali imejiimarisha kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne. Katika Mwaka 2025/2026, Bajeti imezingatia kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara, kuendelea kuhimili athari za majanga, ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko.

### Punguzo la kodi/wakulima watajwa

Katika kipindi hiki cha mvutano wa kibiashara baina ya Mataifa makubwa yanayoendelea kutokana na nchi ya Marekani kutangaza mabadiriko mbalimbali ya kisera kwa lengo la kuimarisha uchumi wake, Tanzania imekuja na tiba kwa wakulima wake.

Kundi hilo limekumbukwa kwa kutolewa kodi kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha miaka mitatu ili kuwajengea uwezo wakulima kuzifikia ndoto zao.
Kingine ni kusamehe kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchini kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mbali na punguzo la kodi kwenye mbolea na mbegu za mafuta zinazozalishwa nchini, Bajeti imeangazia kwenye pembejeo ikiwemo vifaa vya matrekta kama matairi na vitu vingine ili kutoa unafuu kwa wakulima wa Tanzania kulima kwa kutumia zana za kisasa zitakazowaongezea kipato.

### Watalii wapunguziwa kodi

Kati ya miaka yenye neema kwa watalii huenda ikawa ni Bajeti hii ya 2025/2026 kwani Serikali imezifuta na kupunguza kwa kiasi kikubwa baadhi ya kodi na tozo zilizokuwa kero kwa wafanyabiashara na wadau wa masuala ya utalii jambo lililowakatisha tamaa kwani walilazimisha kupandisha viwango na hivyo kuwanyima haki wageni. Lengo ni kuongeza mapato kupitia ongezeko la idadi ya watalii watakaoingia nchini katika kipindi hicho ambapo sheria zimefanyiwa maboresho katika eneo hilo.

Wabunge wanaotoka maeneo ya ukanda wa kitalii wameitaja bajeti hii kwamba ni ya kimkakati na inagusa mahali penye maslahi hasa katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

"Punguzo hilo siyo kuikosesha Serikali mapato ila ni kuiongezea, naona kabisa idadi ya watalii wanakwenda kuongezeka mara dufu hivyo tunategemea mapato yakaongezeke," anasema Mhe. Joseph Tadayo.

Mbunge huyo kutoka Jimbo la Mwanga anasifia uamuzi wa Serikali akisema siyo kuwasikiliza Wabunge pekee, bali imefanya utafiti na kubaini wapi panavuja na wamepaona na kuziba. Tadayo anasema kuwa Wananchi wategemee neema na mambo mazuri kwani hakuna mahali palipowekewa ugumu katika utekelezaji wa Bajeti hii.

### Miamala ya Simu/Benki yaboreshwa

"Mheshimiwa Spika, alikadharika, Benki imetoa mwongozo kwa watoa huduma za fedha kuhusu kushusha gharama za miamala kutoka Benki kwenda mitandao ya simu na kutoka mitandao ya simu kwenda Benki," alisema Dkt. Mwigulu.

Kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri, ahueni hii itakayoanza kutumika kuanzia Julai Mosi Mwaka huu, gharama zinapungua kutoka Sh. 12,000 hadi gharama isiyozidi Sh. 5,000 ambapo Bajeti inalenga kulinda maslahi ya watumiaji na kuhakikisha unafuu kwa gharama za wananchi.

Serikali imeahidi kuendelea kushirikiana na watoa huduma wote katika sekta ya fedha katika kufanya mageuzi ya kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika uchumi. Kwenye eneo hilo ambalo linawagusa wananchi wengi, Serikali imepanga kuzindua mkakati wa kukuza matumizi ya huduma za fedha na malipo kwa njia ya kidigitali kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mkakati huo unalenga kufanya maboresho ya sera, sheria na

miongozo inayohusu malipo ya kidigitali hivyo, Waziri ameagiza watoa huduma za fedha kuendelea kupunguza gharama za miamala ya kidigitali ili kuwezesha wananchi kufanya malipo kwa njia hiyo lakini kwa gharama nafuu.

### Maoni ya Wabunge

Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ester Matiko anasema Bajeti ya Mwaka 2025/2026 siyo Bajeti ya Serikali bali ni Bajeti ya wananchi kwa kuwa imewagusa moja kwa moja wananchi wa hali ya chini.

Mhe. Matiko amesema kila ukurasa uliosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba umebeba maana kubwa kwa wananchi lakini akasisitiza nidhamu katika matumizi ya kile kitakachokusanywa.

"Kwa mfano, Serikali ilikuja mbele ya Kamati ya Wabunge wote na pendekezo la zaidi ya Sh. trilioni 57, lakini ndani ya Bunge Waziri amesema kiwango pungufu, hii imebeba ujumbe kuwa wameona kuna haja ya kwenda na uhalisia siyo maneno," amesema Matiko.

Mbunge huyo anasema Bajeti imelenga zaidi maendeleo ya watu ikiwemo bidhaa za viwandani ambazo zinazalishwa na malighafi kutoka ndani ya nchi jambo linalokwenda kuwainua kiuchumi wakulima.

Amesema kwa Mwaka 2025/2026 wananchi wategemee mema zaidi na mema mazuri yanakuja akigusia namna Bajeti ilivyogusa eneo la afya bila kutegemea misaada kutoka kwa wahisani ambao anasema mara nyingi huchelewesha Maendeleo ya nchi.

Mgombea wa Kiti cha Urais kwa Chama cha ADC kwenye uchaguzi Mkuu ujao, Ndg. Mutamwega Mugaywa anasema Bajeti ni nzuri na imegusa maeneo muhimu isipokuwa inapaswa kusimamiwa kikamilifu ili iweze kutekelezeka.

Mugaywa ambaye alikuwa miongoni mwa wanasiasa walioshiriki wakati wa uwasilishwaji wa Bajeti hiyo Juni 12, 2025 anasema malengo ni mazuri isipokuwa yanapaswa kuwa na uhalisia na ikitokea hivyo itakuwa ni jambo jema na lenye kuwapa matumaini wananchi.

### Spika aita mdahalo kuhusu Bajeti

Ili kuwapa uelewa Wabunge, Spika wa Bunge Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson aliamua kuwaita Wabunge na wataalamu ili kuzungumzia kwa mapana kuhusu Bajeti na jinsi itakavyotekelezwa.

Mpango huo ni kwa mara ya kwanza katika historia ya Bunge na kwa sehemu kubwa ulionekana kuwa na mafanikio mazuri kwa kuwa Wabunge walichongewa njia ya nini wanaweza kufanya kwenye michango yao ili kuboresha. Kitendo hicho kiliwavutia Wabunge na ndipo Mbunge wa kuteuliwa Mheshimiwa Dkt. Bashiru Ally aliomba jambo hilo lisiwe hiyari hata kwa Bunge lijalo kwani linawapa uhuru zaidi Wabunge baada ya kuwa na uelewa kwa kila kipengere ndipo wanaweza kuishauri zaidi Serikali.



Mabalozi, Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa na Viongozi wengine wa Kitaifa wakifuatilia uwasilishwaji wa Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka kwa Fedha 2025/2026 Bungeni, Jijini Dodoma

# *Dkt. Tulia* - Tuimarishe Mshikamano wa Jumuiya ya A. Mashariki kupitia matumizi ya Teknolojia



Spika wa Bunge la Tanzania Mhe. **Dkt Tulia Ackson** akihutubia Mkutano wa 19 wa Maspika wa Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 24 Mei, 2025 Jijini Dar es Salaam.

> **Matumizi ya Akili Unde ni jambo la kimaendeleo katika mazingira ya sasa ya maendeleo ya Afrika Mashariki. Tunaweza kuwa na mweleko wa Jumuiya mpya kwa kuwa na miundombinu ya kisasa ya taarifa na maarifa inayotumia teknolojia,"**
>
> *Dkt. Tulia Ackson*

Na. **Omary Machunda**

SPIKA wa Bunge la Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ametoa wito kwa Maspika wenzake kutoka nchi za Afrika Mashariki kuimarisha umoja na mshikamano katika kufanikisha upatikanaji wa maendeleo kupitia matumizi ya teknolojia ya kisasa ya akili unde.

Akihutubia Mkutano wa 19 wa Maspika wa Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 24 Mei, 2025 Jijini Dar es Salaam, alisema Mkutano huo una jukumu la kufanikisha ndoto na matumaini ya watu zaidi ya milioni 300 wa Afrika Mashariki wanaohitaji kuona maendeleo yakifikiwa kwa haraka katika sekta mbalimbali kwenye nchi zao.

"Waheshimiwa Wajumbe wa Mkutano huu muhimu, kutokana na maendeleo makubwa ya teknolojia yaliyopo kwa sasa duniani, ni vizuri tuanze kwa kuimarisha mpango wa Bunge mtandao ili ufanye kazi sambamba na matumizi ya akili unde kwa lengo la kukidhi mahitaji ya sasa katika eneo la teknolojia na kwa kufanya hivyo hakuna yeyote miongoni mwetu atakayeachwa nyuma," alisema.

Awali katika Mkutano huo, Dkt. Tulia alipongeza maendeleo yaliyopatikana katika sekta ya teknolojia miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuziomba nchi hizo ziongeze uwekezaji katika eneo la utafiti wa matumizi ya akili unde ili kupiga hatua za maendeleo kwa haraka zaidi kutokana na ufanisi wa teknolojia hiyo.

"Hapa Tanzania kwa mfano, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia mfumo unaoongozwa na akili unde kimetoa suluhisho katika sekta ya maji, nchini Rwanda, Kituo cha Mapinduzi ya Nne ya Viwanda kinaandaa mifumo ya udhibiti ubora viwandani wakati nchini Kenya, kupitia matumizi ya akili unde wanaandaa kikosi kazi kitakachoboresha sera mbalimbali nchini humo", alisema.

Dkt. Tulia alieleza kwamba, katika historia ndoto za waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walitamani kuona Afrika Mashariki iliyoungana, yenye mshikamano, inayojitegemea na yenye sauti moja katika dunia ya ushindani kupitia uhuru wa kisiasa, kiuchumi, mshikamano wa kijamii, miundombinu ya reli na barabara ya pamoja kama nguzo muhimu za kuunganisha Jumuiya.

Alisisitiza kuwa, katika karne ya 21 matumizi ya akili unde siyo anasa bali ni jambo la msingi na la lazima.

"Matumizi ya akili unde ni jambo la kimaendeleo katika mazingira ya sasa ya maendeleo ya Afrika Mashariki. Tunaweza kuwa na mwelekeo wa Jumuiya mpya kwa kuwa na miundombinu ya kisasa ya taarifa na maarifa inayotumia teknolojia," alisema.

Aliongeza kwamba fursa ni nyingi iwapo watashirikiana kwa dhati na ni wajibu wao kutetea maslahi ya wananchi wanao wawakilisha.

Dkt. Tulia pia alisema ikiwa reli ya zamani iliunganisha bandari na miji, leo hii teknolojia ya akili unde inaweza kuunganisha wananchi wa Afrika Mashariki katika mambo mbalimbali kama biashara, elimu, afya na utawala bora pasipo mipaka ya kijiografia.

"Kwa leo, mipaka si ya ardhi, ni mipaka ya maarifa, data, lugha, na teknolojia. Kulinda taifa leo si tu kulinda mipaka ya ramani bali ni kulinda mipaka ya akili zetu, taarifa zetu na uwezo wetu wa kujitawala katika zama za akili unde," alieleza.

Dkt. Tulia aliwakumbusha pia Waheshimiwa Maspika wa Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wasibaki kuwa walinzi wa kivuli cha historia bali warithi wa mwanga wa maono na kwamba, ni wakati wao wa kuwasha tochi, kuangaza njia na kuongoza kizazi kuelekea Afrika Mashariki inayojivunia umoja, maendeleo na utu.

Aliwaasa Maspika kwa umoja wao wakubali wajibu wao wa kusukuma mbele ajenda ya kuwa na taasisi bora za kisasa na zinazowajibika ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Aliwaeleza pia Maspika hao kwamba wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuimarisha Taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuhakikisha kuwa watu wa Jumuiya hiyo hawaioni kama taasisi inayojitawala kutoka Arusha, bali kama uhalisia hai unaoleta mabadiliko chanya katika maisha yao ya kila siku.

Hivyo alisema Maspika hao wana wajibu wa kushughulikia changamoto zinazowakabili wananchi kwa kujitoa kwa dhati.

Aliwaeleza kuwa, wajibu huo wa heshima wanaweza kuutekeleza vyema zaidi pale unapojengwa juu ya maarifa thabiti na uelewa wa kina wa mahitaji halisi ya watu.

Aliongeza kwamba kazi yao kama Wabunge huimarika wanapojadili masuala yanayowagusa wanaowawakilisha ndani ya Bunge kwa kujikita katika uhalisia wa maisha ya wananchi.

Kwa ujumla, Dkt. Tulia aliwafahamisha Maspika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba wasikumbukwe tu kama watunga sheria bali wakumbukwe kama wachongaji wa njia za baadaye, wahifadhi wa maono ya Jumuiya, waunganishaji wa watu wa mataifa tofauti na walinzi wa maslahi ya raia wao katika zama hizi za mabadiliko ya haraka ya kidunia.

**"Dhamira ya Tanzania kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki itaendelea kuwa thabiti, bila kujali mabadiliko ya kisiasa na itaendelea kudumisha misingi ya umoja, amani na ustawi wa pamoja."**



**Dkt. Tulia aliwafahamisha Maspika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba wasikumbukwe tu kama watunga sheria bali wakumbukwe kama wachongaji wa njia za baadaye, wahifadhi wa maono ya Jumuiya, waunganishaji wa watu wa mataifa tofauti na walinzi wa maslahi ya raia wao katika zama hizi za mabadiliko ya haraka ya kidunia.**

Aidha, aliwajulisha kuwa Bunge la 12 la Tanzania linamaliza muda wake na Tanzania itaingia katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025.

Alisema dhamira ya Tanzania kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki itaendelea kuwa thabiti, bila kujali mabadiliko ya kisiasa na itaendelea kudumisha misingi ya umoja, amani na ustawi wa pamoja.

Aliwashukuru kwa fursa ya kuhudumu pamoja nao kama Spika wa Bunge na alieleza kujivunia kushirikiana na viongozi wenye maono na moyo wa kuleta maendeleo ya Afrika.

Alieleza kuwa kila walipokutana, walikumbushana kuwa Afrika si mkusanyiko wa mataifa tu, bali ni jumuiya yenye hatima moja.

Aliwaomba Maspika kama Mabalozi wa ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuendelea kusimamia misingi ya kuwa wamoja kwa kuhakikisha uchumi unawahudumia wanadamu kwa utu na kwa kuwa na uhusiano wa kina kati ya demokrasia na maendeleo kwa azma za kuwatumikia wananchi.

Aidha, aliwarai waendelee kuwa walinzi wa amani, maendeleo na muungano kwa mshikamano na aliwakumbusha maneno ya Hayati Dkt. Kwame Nkrumah ambaye alisema: "Hatutazami Mashariki wala Magharibi, tunatazama mbele."



Spika wa Bunge la Tanzania, Mhe.**Dkt Tulia Ackson** (watatu kutoka kushoto waliokaa) akiwa kwenye picha ya pamoja na Maspika wengine wa Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (waliokaa) pamoja na Makatibu wa Mabunge hayo ( waliosimama) wakati Mkutano wa 19 wa Maspika wa Mabunge ya Nchi Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 24 Mei, 2025 Jijini Dar es Salaam.

> **Tuendelee kuwa wamoja ili kufanikisha malengo tuliyojiwekea ya kujenga Jumuiya yenye Umoja, Mshikamano na Maendeleo kupitia kwa viongozi wetu wanaotuongoza ikiwemo Marais, Baraza la Mawaziri, pamoja na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki**
>
> Spika wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Mhe **Joseph Ntakirutimana**



**Sudani Kusini inajidhatiti kuhakikisha inashiriki katika kutekeleza mikakati ya Jumuiya inayolenga kuimarisha ushirikiano na mshikamano miongoni mwa nchi zao kwa lengo la kuleta amani, usalama na maendeleo kwa watu wa Afrika Mashariki.**

*Spika wa Bunge la Serikali ya Mpito ya Sudan Kusini Mheshimiwa Jemma Nunu Kumba*

Alisema, Sudani Kusini inajidhatiti kuhakikisha inashiriki katika kutekeleza mikakati ya Jumuiya inayolenga kuimarisha ushirikiano na mshikamano miongoni mwa nchi zao kwa lengo la kuleta amani, usalama na maendeleo kwa watu wa Afrika Mashariki.

### Spika wa Bunge la Seneti la Kenya

Naye Spika wa Bunge la Seneti la Kenya, Mheshimiwa Amason Jeffah Kingi, aliyaasa Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kushirikiana kwa ukaribu zaidi ili kupambana na changamoto za kimazingira zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa kwa kutumia mbinu za kisasa ikiwemo kuimarisha matumizi ya nishati safi miongoni mwa nchi wanachama.

### Spika wa Bunge la Rwanda

Spika wa Bunge la Rwanda, Mheshimiwa Gertrude Kazarwa, alisisitiza umuhimu wa Maspika hao kukutana mara kwa mara ili kubadilishana uzoefu juu ya namna bora ya kufanikisha mchango wa Mabunge katika kuleta maendeleo ya watu wa Afrika Mashariki.

Mkutano wa 19 wa Maspika wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Hyatt Regency Hotel Jijini Dar es Salaam tarehe 24 Mei, 2025 ulitanguliwa na Mkutano wa Makatibu wa Bunge uliofanyika kwa siku mbili, tarehe 22 na 23 Mei, 2025.

### Spika wa Bunge la EALA

Akizungumza katika mkutano huo wa ngazi ya juu kwa Maspika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Mheshimiwa Joseph Ntakirutimana alizitaka nchi wanachama kusaidiana pale inapohitajika ili kufikia malengo ya upatikanaji wa maendeleo kwa nchi zote za Afrika Mashariki.

"Tuendelee kuwa wamoja ili kufanikisha malengo tuliyojiwekea ya kujenga Jumuiya yenye umoja, mshikamano na maendeleo kupitia kwa viongozi wetu wanaotuongoza ikiwemo Marais, Baraza la Mawaziri, pamoja na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema.

### Spika wa Bunge la Sudan Kusini

Kwa upande wake Spika wa Bunge la Serikali ya Mpito ya Sudan Kusini Mheshimiwa Jemma Nunu Kumba aliwahakikishia Maspika wa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa Serikali ya Sudan Kusini inazingatia suala la uwepo wa amani na usalama katika nchi hiyo pamoja na nchi nyingine majirani kama inavyoelekezwa kwenye Mkataba wa Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

# Usikilizaji na Upokeaji wa Maoni ya Umma katika Mchakato wa Kibunge

**Kihistoria, desturi ya kibunge kusikiliza maoni ya umma, inaendana na historia ya taratibu za Bunge duniani. Kwa nchi za Jumuiya ya Madola kama Tanzania, historia hiyo inaweza kuhusianishwa na chimbuko na maendeleo ya kibunge yaliyoanzia nchini Uingereza.**



Na. **Athuman Hussein**, *ndc*
a.brambati@bunge.go.tz

Usikilizaji na upokeaji wa maoni ya umma ni desturi ya kibunge ya kuwa na mikutano rasmi ambapo umma unakaribishwa kutoa maoni au mawazo kuhusu muswada wa sheria au jambo lingine lolote linalofanyiwa kazi Bungeni. Desturi hii inalenga kuushughulisha umma (public engagement) kwenye masuala yanayofanyiwa kazi na Bunge. Kwa utaratibu huo, ruhusa ya jumla inatolewa kwa watu au taasisi kuwasilisha mtazamo, maoni na ushahidi juu ya suala hilo.

Madhumuni ya makala hii ni kufafanua desturi ya kibunge ya kusikiliza maoni ya umma. Vilevile, makala hii inakusudia kuonesha usuli wa desturi hiyo katika uendeshaji wa Bunge la Tanzania bila kusahau ufafanuzi wa namna inavyofanyika.

Kwa kufanya hivyo, wasomaji watawezeshwa kupata msingi wa Bunge kusikiliza na kupokea maoni ya umma, sanjari na kunga'amua vigezo na masharti yanayozingatiwa kwenye desturi hii. Njia inayotumika kufanikisha madhumuni hayo ni ubainishaji wa miongozo (prescriptive approach) na usimulizi (narrative approach) inapobidi.

Chimbuko la desturi ya Bunge kusikiliza na kupokea maoni ya umma ni misingi ya demokrasia inayotokana na uliberali (liberalism) lakini kwa kuzingatia mtazamo wa kiyakinifu (Realism). Uliberali ni mtazamo wa kisiasa unaosisitiza demokrasia, uwazi na ushiriki wa wananchi katika uamuzi wa masuala ya uendeshaji wa nchi. Mtazamo huo unachukulia desturi ya kusikiliza na kupokea maoni ya umma kama nyenzo ya kuimarisha demokrasia na uamuzi wa kibunge.

Uyakinifu kwa upande mwingine, ni mtazamo wa kisiasa unaozingatia maslahi ya kiutawala katika uhusiano na ushirikiano wa kimataifa pamoja na mikakati muhimu ya uhai wa taifa kwa siasa za ndani na za nje ya nchi. Kwa mtazamo huu, desturi ya kusikiliza maoni ya umma ni mbinu kuimarisha taswira ya utawala na kuzingatia inavyostahili hali ya siasa. Msisitizo wa mtazamo huu upo kwenye umma kustahili ushirikishwaji.

Kwa uyakinifu, uamuzi kuhusu jambo linalofanyiwa kazi kwa kupokea maoni ya umma ni jukumu la mamlaka inayohusika,

wala si la watoa maoni. Kwa maneno mengine, usikilizaji wa maoni ya umma hauzuii uamuzi kuhusu jambo linalotolewa maoni.

Hata hivyo, umuhimu wa maoni ya umma, unaendelea kuwepo kwa kuwa ni jambo linaloboresha hatua zinazochukuliwa kwa maslahi ya umma. Thamani ya desturi hii kwa mtazamo wa kiyakinifu ni kufanikisha mchakato wa kufikiri kuhusu masuala ya umma kwa namna inayojikita katika ukweli na mantiki kulingana na mazingira halisi.

Kwa ujumla, mitazamo hiyo kwa pamoja inachukulia desturi ya kusikiliza maoni ya umma kama njia au mbinu ya kuboresha michakato ya uamuzi. Njia hii inajenga uhusiano mzuri kati ya viongozi na wanaoongozwa na wawakilishi na wanaowakilishwa.

Kihistoria, desturi ya kibunge kusikiliza maoni ya umma, inaendana na historia ya taratibu za Bunge duniani. Kwa nchi za Jumuiya ya Madola kama Tanzania, historia hiyo inaweza kuhusianishwa na chimbuko na maendeleo ya kibunge yaliyoanzia nchini Uingereza.

Mifumo ya awali ya uendeshaji wa Bunge ilianza bila kuwa na ushiriki wa umma. Baadaye uamuzi wa kibunge ukaanza kufanyika kwa namna mbalimbali ya kushirikisha watu lakini kwa kiwango kidogo. Mfano, kuwaita wataalamu watoe maoni yao na watu wengine watoe ushahidi kwenye Kamati za Bunge.

Sababu ya kukosekana kwa ushiriki wa umma wakati huo ni za kihistoria. Chombo kilichokutana kama Bunge wakati



**“Mifumo ya awali ya uendeshaji wa Bunge ilianza bila kuwa na ushiriki wa umma. Baadaye uamuzi wa kibunge ukaanza kufanyika kwa namna mbalimbali ya kushirikisha watu lakini kwa kiwango kidogo. Mfano, kuwaita wataalamu watoe maoni yao na watu wengine watoe ushahidi kwenye Kamati za Bunge”**





huo kilihusisha matabaka ya juu pekee na hivyo kilijielekeza kukidhi mtazamo wa watawala na si wa umma. Kwa msingi huo, hakukuwa na mantiki ya kuushirikisha umma.

Kukua kwa demokrasia na kuendea kwake kwa pamoja na mapinduzi au mageuzi ya kisiasa huko Uropa na Amerika ni mambo yaliyosisimua maendeleo ya desturi ya kibunge ya kusikiliza maoni ya umma. Mnamo karne ya 18 hadi 19, mabunge yalianza kuwa ya uwakilishi zaidi kuliko tabaka la ushauri kwa watawala.

Pamoja na hatua hiyo, ushiriki wa moja kwa moja wa umma katika uamuzi wa kibunge, ulibaki kuwa mdogo. Sababu yake ni kuwa, mabunge hayo yalichukua sura ya uwakilishi na uamuzi wake ulifanyika kwa niaba ya watu na umma. Kwa mantiki hiyo, maslahi ya umma yalihitaji kupewa kipaumbele.

Maendeleo ya demokrasia ya kikatiba mnamo karne ya 20, yaliweka msisitizo mkubwa katika desturi ya kuushirikisha umma kwenye masuala ya maslahi ya pamoja. Baada ya Vita vya Pili vya Dunia, taasisi za kikatiba ziliimarika zaidi na harakati madhubuti za haki za binadamu ziliongezeka, hali iliyochochea kutambuliwa rasmi kwa ushiriki wa wananchi kama haki ya msingi katika uendeshaji wa mambo ya nchi.

Katika muktadha huu, mabunge ambayo ni vyombo vya uwakilishi wa wananchi, yalichukua jukumu muhimu katika kufanikisha ushirikishwaji huo. Vikao vya Kamati za Bunge vikaanza kufanyika ili kusikiliza na kupokea maoni ya wadau katika umma.

Vichocheo vya mabadiliko hayo vilitokana na msisitizo wa kiuendeshaji wa masuala ya umma uliotoa wito wa kuwa na uwazi, uwajibikaji na ushirkishwaji wa umma katika uendeshaji wa nchi. Hatua hiyo ilikuwa ikiendelea kuimarika kadiri ya mabadiliko ya mifumo ya uendeshaji wa nchi.

Nchini Tanzania desturi ya usikilizaji wa maoni ya umma katika mchakato ya Bunge imepitia hatua mbalimbali za kihistoria. Kuna wakati Bunge halikuwa na desturi ya kualika umma na kupokea maoni lakini baadaye, likaanza kupokea maoni ya umma kwa kuwaalika wadau.

Historia inaonesha kuwa kabla ya mwaka 2004, Kamati za Bunge zilianza kualika wadau kwa ajili ya kupokea maoni ya umma kuhusu miswada ya sharia. Wakati huo, utaratibu wa kupokea maoni ulikuwa kwa miswada ya sheria na ulitegemea utashi wa Kamati ya Bunge iliyokuwa na jukumu hilo. Baadaye Kanuni za Bunge zikajumuisha desturi ya Kamati za Bunge kupokea maoni ya umma.

Toleo la Kanuni za Bunge lililoanza kubainisha suala la kupokea maoni ya umma, ni Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2000. Kanuni ya 69 (2) ya Kanuni za Bunge, mwaka 2000 iliruhusu Kamati iliyopelekewa Muswada kumwalika mtu yeyote afike mbele ya Kamati. Madhumuni ya mtu huyo kufika kwenye Kamati ni kutoa maoni yake kuhusu muswada unaohusika ili kuisaidia Kamati hiyo katika uchambuzi. Matoleo yaliyotangulia hayakuzungumzia chochote kuhusu desturi hiyo.

Katika ufafanuzi wa Kanuni toleo la mwaka 2000, kuna mambo mawili makubwa. **Kwanza**, ilielezwa kuwa "Kamati yaweza" kumwalika mtu maneno ambayo yanaonesha kwamba, usikilizaji na upokeaji wa maoni ya umma si lazima. Kanuni imeipa Kamati hiari ya kupokea maoni ya umma.

**Pili**, ruhusa kwa Kamati kualika wadau au mtu mwingine yeyote, iliegemezwa kwenye idhini ya Spika. Kanuni hiyo iliruhusu Kamati kuwaalika watu wafike kutoa maoni, kwa masharti kwamba, iwe imepata idhini ya Spika kutoa mwaliko huo.

Kwa ujumla, ili mtu au watu waalikwe kutoa maoni yao kwenye Kamati, kuna mambo matatu yaliyopaswa kukamilika kwa pamoja. Mambo hayo ni **mosi**, Kamati kuwa imepelekewa Muswada wa Sheria baaada ya kusomwa mara ya kwanza. **Pili** ni Kamati kuwa na utashi wa kufanya hivyo. Kama haina utashi inaweza kuendelea. **Tatu** ni idhini ya Spika.



Kwa upande wa idhini ya Spika, ilitakiwa kwa mambo matatu. Kwanza, kuhusu mtu anayealikwa. Pili ni madhumuni ya kumwalika mtu au watu na tatu ni wakati wa kukutana kwa ajili kupokea maoni.

Tathmini ya jumla kuhusu desturi ya kusikiliza maoni ya umma kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2000, inaonesha mambo makuu mawili. Mambo hayo yanahusu kutumika kwa desturi hiyo kwa masharti yake na mawanda ya desturi yanyewe.

Masharti ya kutumika kwa desturi hiyo yalianza kuingizwa kwenye Kanuni mwaka 2000. Utekelezaji wake ulitegemea muono wa Kamati na idhini ya Spika. Iwapo Kamati haikuona umuhimu, ingeliweza kuacha na iwapo Spika haidhinishi, Kamati isingelisikiliza maoni ya umma.

Kuhusu mawanda ya kutumika kwa desturi hiyo, Kanuni ilifunga kwenye muswada wa sheria. Suala linalohusu hoja ya kuridhia mikataba (ratification) au kuruhusu kuingia mkataba baadaye (accession), halikuguswa na desturi ya kusikiliza maoni ya umma iliyotambuliwa na Kanuni za Bunge, Toleo la 2000.

Kadhalika, Kanuni hazikugusa utaratibu wa Kamati Teule kusikiliza maoni ya umma. Hivyo ruhusa kwa Kamati Teule kusikiliza maoni ya umma haikuwepo. Bunge la Tisa lililoongozwa na Hayati Samwel Sitta, Mbunge wa Urambo, lilichakata mabadiliko makubwa ya Kanuni. Hadi kufikia mwaka 2007, Bunge likatunga Kanuni za Kudumu za Bunge chini ya Ibara ya 84 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Toleo hilo la Kanuni liliweka desturi ya kusikiliza maoni ya umma kwa utaratibu wa kupokea maoni ya wadau, kuwa jambo la lazima. Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 ilibainisha sharti hilo. Aidha, Kanuni ya 114 (9) ya Kanuni , mwaka 2007, ilitaka Kamati kuwa na utaratibu wa kualika wadau wakati inaposhugulukia Muswada au jambo lingine lolote.

Kanuni hiyo, iliongeza wigo wa mambo yanayoweza kufanyika kwa kupokea maoni ya wadau. Ilitaka Kamati ipokee na kusikiliza maoni ya umma kwa utaratibu wa maoni ya wadau kuhusu jambo lolote linalofanyiwa kazi na Kamati.

Tathmini ya Toleo la 2007 inaonesha mambo makubwa manne yaliyoboreshwa kuhusu usikilizaji wa maoni ya umma. **Mosi** ni kuiweka desturi ya kusikiliza maoni ya umma, kuwa jambo la lazima kwa Kamati iliyopelekewa muswada. Kabala ya hapo ilikuwa ni hiari.

**Pili** ni kuondoa sharti la idhini ya Spika ili kusikiliza maoni ya umma. Awali uamuzi wa Kamati kusikiliza maoni ya umma, ulitegemea idhini ya Spika. Kwa mabadiliko ya 2007, idhini haikuwa tena ni sharti.

**Tatu**, kuongezeka kwa wigo wa kutumika kwa desturi ya kusikiliza maoni ya umma kwa utaratibu wa wadau. Kwa mabadiliko ya mwaka 2007, desturi ya kusikiliza maoni ya wadau ikawa lazima kwa miswada na jambo lingine lolote linaloshughulikiwa na Kamati.

**Nne**, Kanuni zimeongeza ufafanuzi kuhusu njia ya kutoa mwaliko ambapo zimetajwa njia mbili: Moja ni barua ya mwaliko na nyingine ni kutoa matangazo. Baada ya mabadiliko hayo ya mwaka 2007, mabadiliko mengine ya mwaka 2013, mwaka 2026, mwaka 2020 na mwaka 2023 yaliendelea na utaratibu wa kutambua desturi ya kusikiliza maoni ya umma.

Hadi sasa, desturi hiyo inatumika na inaleta mafanikio makubwa katika michakato ya kibunge. Kwa kawaida kila muswada wa sheria, unapopelekwa kwenye Kamati, wadau na umma kwa ujumla hujulishwa na kualikwa wafike mbele ya Kamati.

Kwa mfano, tarehe 10 Novemba, 2023, miswada miwili ilisomwa mara ya kwanza kwa mujibu wa Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023. Miswada hiyo ni Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023. Mwingine ni Muswada wa Sheria wa Tume ya Uchaguzi wa Mwaka 2023.

Baada ya miswada hiyo kusomwa Mara ya Kwanza, ilipelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Kamati hiyo, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2023 inayohusu Kamati iliyopelekewa muswada, kualika watu wotoe maoni. Kanuni nyingine ni Kanuni ya 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayotaka shughuli za kawaida za Kamati ziendeshwe kwa uwazi na Kamati ialike wadau.

Kwa msingi huo, Kamati ilifanya mikutano ya kupokea maoni ya umma tarehe 06 na 8 – 10 Januari, 2024. Wananchi zaidi ya 1700 waliripotiwa kufika kwenye Kamati kwa ajili ya kutoa maoni. Kadhalika, Asasi Zisizo za Serikali (AZISE) thelathini na moja, zilishiriki kutoa maoni. Asasi za Kiraia (AZAKI) nyinine zaidi ya 400 zilituma maoni yao. Viongozi wa dini kutoka taasisi tatu: TEC, CCT na BAKWATA nao walialikwa na kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao.

Hatua hiyo ya kupokea na kusikiliza maoni, hufuatiwa na mjadala wa Kamati kwa kuchambua maoni ya wadau kwa kigezo cha muswada ulivyo. Kutokana na hatua hiyo, Kamati huchanganua na kupata hoja za kuzitumia wakati wa mchakato wake wa kushughulikia miswada.

Maelezo yate hayo, yanaungwa mkono na kauli kwamba, "Sauti ya mwananchi si kelele mitaani, bali ni chemchemi ya hekima ambayo hufaa kutiririka hadi meza ya uamuzi. Taifa linalosikiliza wananchi wake hujenga si tu sheria, bali uhalali wa utawala wenye mizizi katika mioyo ya watu." Kwa ujumla, fasili ya dhana ya upokeaji na usikilizaji wa maoni ya umma pamoja na chimbuko au maendeleo yake kwa ujumla vimeelezwa. Historia ya desturi ya kupokea maoni ya umma katika Bunge la Tanzania imefafanuliwea.





# Mchakato Wa Kutunga Sheria Katika Bunge

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. **Hamza Johari** akizungumza Bungeni

Na. **Ruth Makungu**
r.makungu@bunge.go.tz

**Katika mfumo wa utawala wa kidemokrasia, utungaji wa sheria ni msingi muhimu wa kuhakikisha haki, amani na maendeleo ya jamii. Sheria huongoza maisha ya watu kwa kuweka mipaka ya kile kinachoruhusiwa na kinachokatazwa.**

**Sheria hubainisha adhabu kwa ukiukwaji wa masharti kuhusu mipaka ya ruhusa na makatazo. Katika muktadha wa Tanzania, Bunge ndicho chombo kikuu cha kutunga sheria kwa niaba ya wananchi kupitia mchakato rasmi unaojumuisha uwasilishaji, mjadala, marekebisho na hatimaye kupitishwa kwa miswada kuwa sheria.**

Makala hii inakusudia kufafanua kwa kina hatua mbalimbali za mchakato wa utungaji wa sheria ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ufafanuzi huo unaanzia kuwasilishwa kwa muswada hadi kutangazwa rasmi kuwa sheria inayotumika kisheria. Lengo ni kutoa uelewa wa jumla kwa wasomaji kuhusu namna sheria zinavyotungwa na umuhimu wa mchakato huo katika kuimarisha utawala wa sheria nchini.

Mchakato wa kutunga sheria katika Bunge la Tanzania huanza kwa pendekezo la sheria ambalo huweza kuletwa Bungeni na Serikali au Mbunge au Kamati. Pendekezo la sheria ambayo haijapitishwa kwa ukamilifu huitwa muswada. Muswada ukishapitishwa kwa ukamilifu na Bunge na kupata idhini ya Rais huitwa sheria.

Mchakato wa kutunga sheria unajumuisha hatua zilizopangwa na kuwekewa masharti katika Kanuni za Bunge. Kwa sasa Kanuni ya 93 hadi 106 za Kanuni za Kudumu za Bunge zimeweka bayana hatua ambazo zinapaswa kufuatwa kikamilifu ili kuhakikisha uhalali na ufanisi wa sheria itakayotungwa.

Hatua ya kwanza inahusu Muswada wa sheria kutangazwa rasmi kisheria. Kanuni ya 93 ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Tanzania, imeweka sharti kwamba, muswada wowote unaokusudiwa kufanyiwa kazi na Bunge utangazwe kwenye Gazeti la Serikali. Lengo la hatua hii ni kuweka uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa kutunga sheria kwa kuufahamisha umma kuhusu sheria inayokusudiwa kutungwa na pengine kutoa nafasi ya kuanza kujiandaa kutoa maoni kabla sheria haijaidhinishwa.

> **Ieleweke kuwa, muswada wa sheria ukishasomwa mara ya kwanza hakuna mjadala wala kupiga kura katika hatua hiyo. Kinachofuatia ni kufanyiwa kazi na Kamati inayohusika ambayo imetajwa katika Kanuni ya 136 (14) ya Kanuni za Bunge.**

***Kamati hiyo, huchambua kwa undani kila kipengele cha muswada ili kugundua upungufu, dosari, athari au changamoto zinazoweza kutokea iwapo muswada huo utapitishwa kama ulivyo.***

Kwa mujibu wa Kanuni, tangazo la muswada wa sheria linapaswa kutolewa na kumfikia Katibu wa Bunge katika muda usiopungua siku ishirini na moja kabla ya muswada unaohusika kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza. Tangazo hilo linapaswa kuonesha muswada mzima ikiwa ni pamoja na maelezo kuhusu sababu na madhumuni ya muswada huo yaliyotiwa saini na Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Muswada wa Sheria wa Serikali unaweza kuandaliwa na kuwasilishwa Bungeni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Waziri. Mwanasheria Mkuu wa Serikali hutekeleza jukumu la kuandaa na kuwasilisha muswada Bungeni kwa sababu ndiye mshauri mkuu wa sheria. Kwa upande wa Waziri, anahusika kuwasilisha muswada wa sheria Bungeni kwa sababu ndiye mwenye dhamana ya kisera katika sekta inayohusika na muswada, sekta ambayo ipo chini ya dhamana yake na hivyo anao uelewa wa kina kuhusu madhumuni, umuhimu na athari za kiutendaji katika sheria inayopendekezwa.

Muswada wa Sheria wa Serikali unaweza kuletwa Bungeni kwa hati ya dharura. Uwezekano huo unakuwepo pale ambapo kuna haja ya kutunga au kurekebisha sheria kwa haraka kuliko inavyowezekana kwa utaratibu wa kawaida. Haraka hiyo iwe inatokana na umuhimu au uzito wa jambo kitaifa kwa maslahi ya umma.

Kwa maelezo hayo, dharura inaweza kuwa inatokana na janga la kitaifa, haja ya haraka kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, utekelezaji wa makubaliano ya kitaifa au mahitaji ya kisheria yanayotokana na uamuzi wa Mahakama. Kwa mazingira hayo, utaratibu wa hati ya dharura huruhusu muswada usomwe na kujadiliwa kwa haraka bila kupitia mchakato wa kawaida. Lengo la ruhusa hiyo ni kuiwezesha Serikali kuchukua hatua stahiki kwa wakati.

Ili Bunge liweze kufanyia kazi muswada uliowasilishwa kwa hati ya dharura, sharti Kamati ya Uongozi iweze kujiridhisha iwapo Muswada unaohusika unastahili kuwasilishwa kwa dharura au haustahili kuwasilishwa kwa dharura. Ikiwa Kamati ya Uongozi itaona kuwa Muswada wa Sheria wa Serikali haustahili kuwasilishwa kwa dharura, itaishauri Serikali ipasavyo.

Halikadhalika, Mbunge yeyote au Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge anaweza kuwasilisha Bungeni Muswada Binafsi wa Sheria pale anapoona kuna hitaji la kisheria linalogusa maslahi ya wananchi au taifa kwa ujumla ambalo halijashughulikiwa na Serikali.

Mbunge au Kamati inayokusudia kuwasilisha muswada Bungeni ni lazima atoe taarifa kwa Katibu wa Bunge. Taarifa hiyo itaeleza jina la muswada unaopendekezwa pamoja na madhumuni ya muswada. Kama ilivyo kwa miswada ya sheria ya Serikali, muswada binafsi nao utatangazwa katika Gazeti la Serikali isipokuwa kwamba madhumuni yatawekwa saini na Mwenyekiti wa Kamati au Mbunge anayehusika.

Masharti kuhusu muda wa utangazaji wa muswada ya sheria yanaweza kuwekwa kando na kutenguliwa kwa hoja kutolewa na kuamuliwa kama kutawasilishwa Bungeni hati iliyowekwa saini na theluthi mbili ya Wajumbe wote wa Kamati kama ni Muswada wa Kamati. Ikiwa ni Muswada wa Mbunge kuna sharti la kuwepo kwa hati iliyowekwa saini na Wabunge wasiopungua kumi inayoeleza kuwa Muswada Binafsi uliotajwa katika hati hiyo ni wa dharura.

Mazingira ya kuweka kando utangazaji wa muswada binafsi ni kama yale ya Muswada wa Serikali. Kwa hivyo, kuondoa sharti la kutangazwa mapema kunatoa nafasi kwa Bunge kujadili na kupitisha muswada kwa haraka ili kulinda maslahi ya taifa.

Kwa ujumla, masharti ya kushughulikia kwa hatua zote kwa Muswada wa Sheria wa Serikali na Muswada Binafsi yanafanana. Hatua kuu zinazofuatwa katika mchakato wa muswada Bungeni zinahusisha Muswada kusomwa Mara ya Kwanza Bungeni, Muswada kuchunguzwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge inayohusika na Muswada kusomwa Mara ya Pili Bungeni. Hatua nyingine ni Muswada kufikiriwa na Kamati ya Bunge Zima ibara moja baada ya nyingine, Muswada kusomwa Mara ya Tatu Bungeni na kupitishwa, Sheria kupata Idhini ya Rais na Kutangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa Sheria ya nchi.

Hatua zote hizo zina lengo la kutoa nafasi ya kutosha kwa sehemu mbili za Bunge, Wabunge na Rais, kuufanyia kazi kwa makini na kwa undani muswada unaohusika. Kufanya hivyo, kunawezesha utungaji wa sheria itakayotokana na Muswada huo itungwe pasipo kuwa na matatizo yanayoweza kuepukika.

Historia inaonesha kuwa, wakati nchi ilipokuwa katika mfumo wa chama kimoja cha siasa, miswada ya sheria ilikuwa ikisomwa mara mbili tu na kupitishwa. Hatua hii ya miswada kusomwa mara tatu ni miongoni mwa mabadiliko yanayozingatia utawala bora kwa Bunge.

Muswada wa Sheria kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza unalenga kujenga uelewa miongoni mwa Wabunge kuhusu maudhui ya muswada. Kadhalika, hatua hiyo inatoa fursa kwa umma kutaarifiwa kuwa kuna pendekezo la sheria ambalo linaanza katika mchakato Bungeni.




Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. **Hamza Johar**i akizungumza wakati wa Kikao cha Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Kushoto kwake ni Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. **Damas Ndumbaro** na kulia kwake Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhe. **Jumanne Sagini**

**Bunge linapokaa kama Kamati ya Bunge Zima huchambua kwa kina ibara kwa ibara za muswada na kubaini maeneo yanayohitaji marekebisho, kuondolewa au kuboreshwa.**

***Katika hatua hii, wabunge wanaweza kupendekeza marekebisho kwa ibara ya muswada.***

Ieleweke kuwa, muswada wa sheria ukishasomwa mara ya kwanza hakuna mjadala wala kupiga kura katika hatua hiyo. Kinachofuatia ni kufanyiwa kazi na Kamati inayohusika ambayo imetajwa katika Kanuni ya 136 (14) ya Kanuni za Bunge. Kamati hiyo, huchambua kwa undani kila kipengele cha muswada ili kugundua upungufu, dosari, athari au changamoto zinazoweza kutokea iwapo muswada huo utapitishwa kama ulivyo.

Aidha, Kamati imepewa wajibu wa kuwaalika wadau mbalimbali na kupokea maoni ili kuhakikisha kwamba, muswada huo unazingatia maslahi ya umma, unatekelezeka kwa uhalisia na hauleti madhara katika jamii. Ushirikishwaji wa wadau huongeza uwazi, uwajibikaji na ubora wa sheria.

Maoni ya wadau husaidia Kamati kubaini upungufu, changamoto au maboresho yanayohitajika katika sheria inayopendekezwa (muswada). Kushirikishwa kwa wadau kunatokana na Bunge kuzingatia kwamba, sheria itakapotungwa, itawagusa moja kwa moja.

Kamati iliyopelekewa muswada inapokamilisha kazi ya uchambuzi wa muswada hufanya mambo mawili. Mosi, kumjulisha Spika kwa maandishi kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Bunge na pili kuandaa taarifa yenye maoni na ushauri wa Kamati kwa ajili ya kuwasilisha Bungeni wakati wa muswada Kusomwa Mara ya Pili.

Hatua ya Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Pili inahusisha Bunge kufanya tathmini kuhusu madhumuni, dhamira na misingi wa muswada huo. Tofauti na Kusomwa Mara ya Kwanza (ambako ni kutangazwa kwa jina la muswada bila mjadala Bungeni), Kusomwa Mara ya Pili kunahusisha mjadala ndani ya Bunge.

Katika hatua hii, Mbunge au Waziri anapata fursa ya kutoa maelezo ya kina kuhusu muswada na manufaa yake sambamba na kueleza ibara au maneno yaliyotumika yanavyofaa au yasivyofaa. Kamati iliyokuwa inashughulikia muswada nayo itatoa maoni, mapendekezo ya marekebisho au kushauri au kulishawushi Bunge lisiupitishe au liupitishe muswada huo kwa sababu itakayozibainisha. .

Aidha, Kambi ya Walio Wachache Bungeni nayo inaweza kutoa maoni kuhusu muswada huo. Maoni yake yatalenga kulishawishi Bunge kuhusu kuupitisha au kutokuupitisha muswada unaohusika. Maoni yanayotolewa yanapaswa kulilenga Bunge ambalo ndilo lenye jukumu kuhusu muswada unaofanyiwa kazi.

Mjadala wa jumla huanza baada ya mawasilisho na lengo lake si lingine ila kujiridhisha na mantiki, sababu na madhumuni ya mapendekezo, maneno yaliyotumika, masharti yaliyowekwa na maudhui kwa ujumla kabla ya kufaya uamuzi kibunge. Hatua hii ndiyo inayotoa matokeo ambayo yataishia kwenye uamuzi wa Bunge kuupitisha au kutokuupitisha Muswada huo kabla ya kupata idhini ya Rais ambaye ni sehemu ya pili ya Bunge.

Sababu za muswada wa sheria Kusomwa kwa Mara ya Pili zinalenga kuruhusu Wabunge kuchambua kwa kina madhumuni ya muswada, ikiwa ni pamoja na kuelewa nini hasa muswada huo unakusudia kutatua au kuboresha. Ni katika hatua hii, Kamati inaweza kupendekeza mabadiliko au marekebisho katika muswada kabla haujapelekwa kwa hatua kusomwa mara ya tatu. Hatua hii husaidia kuondoa upungufu au dosari na ni sehemu ya msingi ya kutathmini ubora wa muswada. Katika hatua hii mjadala hujikita katika kutathmini madhumuni ya muswada, uhalali (legality), athari za kijamii na utekelezaji. Hapa ndipo hoja zinajengwa na muswada unaweza kubadilishwa kabisa ili kuakisi maoni ya wengi na kuzingatia maslahi ya taifa.

Mjadala wa jumla ukishakamilika, hatua inayofuata ni kuupitia muswada huo ibara kwa ibara. Hatua hii hufanywa na Bunge likiwa limekaa kama "Kamati ya Bunge Zima" na inalenga kuhakikisha muswada unaboreshwa kikamilifu kabla ya kupitishwa kuwa sheria kamili.

Bunge linapokaa kama Kamati ya Bunge Zima huchambua kwa kina ibara kwa ibara za muswada na kubaini maeneo yanayohitaji marekebisho, kuondolewa au kuboreshwa. Katika hatua hii, Wabunge wanaweza kupendekeza marekebisho kwa ibara ya muswada. Kwa mfano, ibara inaweza kubadilishwa lugha, kuongeza ufafanuzi au kurekebisha kifungu kilichogongana au kipingana na sheria nyingine.

Kusomwa kwa Mara ya Tatu ni hatua ya mwisho ya kibunge ya kupitisha muswada wa sheria baada ya kupitia marekebisho yote ya ibara kwa ibara. Hapa, hakuna mjadala wa maudhui ya muswada, hakuna marekebisho yanayoruhusiwa, bali Bunge huamua kwa kura ya ndiyo au hapana kama liukubali muswada wote ulioboreshwa kuwa sheria. Baada ya hatua hii, sheria hiyo inakuwa imepitishwa na Bunge.

Baada ya muswada wa sheria kupitishwa na Bunge katika hatua zote, hatua inayofuata ni kupelekwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuidhinishwa (kutiwa saini). Hii ni sehemu ya utaratibu wa kikatiba unaohakikisha kuwa mihimili yote ya dola yaani Bunge (watunga sheria) na Serikali (watekelezaji) inashiriki katika kutungwa kwa sheria. Rais ambaye ni sehemu ya kwanza ya Bunge, ana uwezo wa kuidhinisha sheria au kutoidhinisha kwa kutumia mamlaka yake.

Rais atasaini Sheria, itatangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali na kuwa Sheria ya nchi. Sheria hii itaanza kutumika baada ya kutangazwa, lakini wakati mwingine inaweza kuwekwa kwenye tarehe maalum kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha Sheria. Na hapa itakuwa hatua ya mwisho wa mchakato.

Makala hii imefafanua maana, madhumuni na hatua za mchakato wa utungaji sheria Bungeni. Imeeleza kuhusu lengo la mchakato huo na mantiki ya kila hatua. Kwa ujumla mchakato wa utungaji wa sheria unalenga kuliwezesha Bunge kutunga sheria kwa namna inayowazingatia watu na maslahi ya umma na taifa. Hakuna hatua inayokusudia tofauti na ufanisi wa Bunge, bali kila moja inawezesha tija ya utekelezaji wa majukumu na madaraka ya Bunge.

# Umuhimu wa Kamati za Bunge Katika Utekelezaji wa Madaraka ya Bunge



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo wakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao

Na. **Athuman Hussein**, *ndc*

a.brambati@bunge.go.tz

*"Kwenye Kamati ndiko ambako kazi halisi ya Bunge (The real work of parliament) hufanyika."*

Hayo yalisemwa na Profesa Gavin Dewry, msomi mashuhuri wa masuala ya utawala wa umma na taratibu za kibunge nchini uingereza. Usemi huo wa mbobezi wa tafiti kuhusu Kamati za Bunge, unaarifu kuwa anayetaka kupata uelewa kuhusu kazi ya Bunge, hana budi kuchimba umuhimu wa Kamati za Bunge katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge.

Kujenga kwenye maelezo hayo, safu hii katika toleo la kumi inaaridhia mfumo wa Kamati za Bunge la Tanzania na mabadiliko yake tangu mwaka 1961 hadi sasa. Kiini cha mkazo katika hilo ni ukweli kuwa desturi na taratibu za uendeshaji wa Bunge hubadilika kadiri ya maendeleo na mageuzi ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiteknolojia katika nchi, kanda na duniani kwa ujumla.

Mfumo mzima wa Kamati za Bunge la Tanzania ni sehemu ya desturi na uendeshaji wa Bunge kwa ujumla, isiyoweza kuepuka matokeo ya mabadiliko na mageuzi. Kwa sababu hiyo, tangu mwaka 1961 hadi sasa, kuna mabadiliko mbalimbali ya mfumo wa Kamati za Bunge.

Kwa minajili ya kuweka msingi wa kufuatilia mtiririko wa maudhui, dhana ya mfumo wa Kamati za Bunge inahitaji kuelezwa. Kwa kuanzia, dhana hiyo inajengeka kwenye fikra kuhusu mfumo. Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) katika Kamusi Kuu ya Kiswahili, Toleo la Tatu, ukurasa wa 619 limefafanua neno "mfumo" kuwa ni namna maalumu ya utendaji. Nao Profesa Mohamed A. Mohamed na Profesa Said A. Mohamed, katika Kamusi ya Visawe, Ukurasa wa 141, wanatujulisha kwamba, sinonimu za neno mfumo ni sera, utaratibu, mpango, mpangilio au mtindo.

Kuyajumuisha hayo, Mfumo wa Kamati za Bunge ni namna, utaratibu na mpangilio wa Kamati za Bunge katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge. Kwa maana hiyo, vijenzi vya Mfumo wa Kamati za Bunge vinajumuisha mambo sita. Ujumbe wa Kamati, mamlaka ya Kamati, uhusiano miongoni mwa Kamati tofauti, muundo wa Kamati, utaratibu wa uendeshaji na mpangilio wa aina za Kamati.

Tangu mwaka 1961 hadi sasa, mabadiliko mbalimbali yalitokea katika ujumbe, mamlaka, utaratibu, muundo, uendeshaji na

> Mwaka 1961, Bunge la Tanganyika lilikuwa na Mfumo wa Kamati za Bunge uliokuwa na aina mbili za Kamati. **Kwanza**, ni Kamati Teule zilizokuwepo kwa mujibu wa Kanuni ya 72 ya Kanuni za Bunge, Mwaka 1961. **Pili**, ni Kamati za Kudumu za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 73 ya Kanuni za Bunge.

mpangilio wa Kamati za Bunge. Matokeo hayo hayakuwa ya kuepukika na yalilenga kuongeza *natija* ya kazi za Bunge.

Kama ilivyosisitizwa na mtopezi au nguli wa masuala ya kibunge, Bwana Erskine May, utendaji wa Bunge hubadilika kadiri muda unavyosonga. Ikumbukwe, kazi halisi ya Bunge hufanyika kwenye Kamati za Bunge.

Kwa ukweli huu, mfumo wa Kamati za Bunge hauna budi kubadilika kulingana na mageuzi katika uendeshaji nchi. Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingine ina asili ya mabadiliko mbalimbali ya Mfumo wa Kamati za Bunge.

Mwaka 1961, Bunge la Tanganyika lilikuwa na Mfumo wa Kamati za Bunge uliokuwa na aina mbili za Kamati. **Kwanza**, ni Kamati Teule zilizokuwepo kwa mujibu wa Kanuni ya 72 ya Kanuni za Bunge, Mwaka 1961. **Pili**, ni Kamati za Kudumu za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 73 ya Kanuni za Bunge.

Mpangilio wa Kamati ulikuwa na Kamati ya Kanuni, Kamati ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Mambo ya Bunge lenyewe na Kamati nyingine yoyote iliyoweza kuagizwa na Bunge iundwe kwa mujibu wa Kanuni ya 73(4) ya Kanuni za Bunge, 1961. Mfumo huo wa Kamati unaonekana dhahiri kujikita zaidi kwenye jukumu la kusimamia matumizi ya fedha za umma na uendeshaji wa Bunge lenyewe. Hakukuwa na mkazo mkubwa katika eneo lingine la majukumu ya Bunge tofauti na ilivyo kwa wakati wa sasa.

Aina nyingine ya Kamati ni Kamati Teule. Kamati hiyo iliundwa kwa hoja maalumu iliyotolewa Bungeni. Utaratibu wa uendeshaji Kamati za Bunge, ulitaka mwenendo wa Kamati hii uwe ni siri. Masharti ya mwenendo huo kuwa siri yanalingana na masharti yaliyopo kwa sasa.

Mambo hayo yalibadilika mwaka 1986 ambapo, Kamati za Kudumu ziliongezeka kutoka tatu hadi Kamati Nane zilizoanzishwa kwa mujibu wa Kanuni 73(1) ya Kanuni za Bunge, 1986. Mfumo huu uliongeza wigo wa Bunge kutumia Kamati katika utekelezaji wa madaraka yake ya kuisimamia Serikali.

Madaraka ya Bunge yaliyotekelezwa kwa kutumia Kamati yalihusu kusimamia masuala ya fedha na uchumi, mambo ya nje ya nchi na mambo ya katiba na sheria. Mengine ni mambo ya siasa na uendeshaji na hesabu za mashirika ya umma. Pamoja nayo, Kanuni ya 73 (2) (d) ya Kanuni za Bunge 1986, ilizitaka Kamati kushughulikia mambo ambayo zitaagizwa na Bunge kuyafanyia kazi.

Jambo moja kubwa katika hayo, linahusu Bunge kutokuwa na Kamati inayohusika na Kanuni za Bunge. Hilo ni tofauti na ilivyokuwa kabla ya mwaka 1986, ambapo Kanuni ya 73(1)(a) ya Kanuni za Bunge, 1961 ilianzisha Kamati inayohusika na Kanuni za Bunge.

Jambo lingine ni hesabu za mashirika ya umma kuwekwa chini ya kamati maalumu ya kudumu. Kanuni ya 73(2)(c) ya Kanuni za Bunge, 1986 ilianzisha Kamati ya Mashirika ya Umma iliyopewa jukumu la kuchambua hesabu za mashirika ya umma.

Mabadiliko hayo ni ongezeko la umuhimu wa Kamati za Bunge ikilinganishwa na mwaka 1961. Ni mabadiliko ambayo yanaendana na maendeleo katika uendeshaji wa shughuli za umma kama vile kuongezeka kwa umuhimu wa jicho la wawakilishi wa wananchi kwenye hesabu za mashirika ya umma.


Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma wakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao


Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii wakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao





Hali hiyo haikusalia hivyo kwa muda wote, bali iliendelea kuitika maendeleo ya kibunge na mabadiliko ya uendeshaji nchi. Mwaka 1994, iliongezeka aina moja ya Kamati za Bunge ambayo ni Kamati za Vyama.

Vilevile, ziliongezeka Kamati nyingine tatu. Kamati hizo ni Kamati ya Huduma na Haki za Wabunge, Kamati ya Ulinzi na Usalama na Kamati ya Huduma za Jamii zilizotajwa kwenye Kanuni ya 89 ya Kanuni za Bunge, 1994.

Mwaka 1996, Bunge lilipofanya mabadiliko ya Kanuni, liligusa mfumo wa Kamati za Bunge kwa kuongeza na kuondoa Kamati za Kudumu. Kamati tatu za Kudumu za Bunge ziliongezeka. Kamati hizo ni Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Makundi Maalumu, Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Mazingira.

Kamati zilizokuwepo kabla ambazo ziliondolewa mwaka 1996 ni Kamati ya Mambo ya Siasa na Kamati ya Mambo Mengineyo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 94 ya Kanuni za Bunge, 1994, Kamati ya Mambo ya Siasa ilikuwa na jukumu la kufikiria miswada ya sheria au jambo lingine lolote linalokabidhiwa kwake na Spika.

Kwa upande wa Kamati ya Mambo mengineyo (*General Purpose Committee*), Kanuni ya 98 ya Kanuni za Bunge, 1994 iliipa jukumu la kushughulikia mambo yoyote ambayo hayako chini ya Kamati nyingine pamoja na kufikiria muswada wa sheria utakaokabidhiwa kwake na Spika. Majukumu yote hayo yalibainishwa kwa kamati nyingine za kudumu baada ya mabadiliko ya mwaka 1996.

Kamati zilizoongezeka kwa mabadiliko ya Mwaka 1996, ni pamoja na Kamati ya Mazingira iliyopewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Mazingira na hatua za kuondoa umasikini. Nnyingine ni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Makundi Mengine Maalumu.

Mabadiliko mengine kwenye mfumo wa Kamati za Bunge yalihusu majukumu ya jumla ya Kamati. Kanuni ya 90 (1) ya Kanuni za Bunge, ilitamka wazi kuwa ni jukumu la kila Kamati ya Kudumu kufuatilia ahadi za Serikali zinazotolewa Bungeni ambazo zinagusa mambo yaliyo katika mamlaka ya Kamati inayohusika. Kwa ujumla wake mambo hayo yaliakisi hali ya usimamizi wa kibunge wa Shughuli za Umma.

Mwaka 1998, Bunge lilifanya mabadiliko ya Kanuni ili kuakisi hali ya jumla ya uendeshaji wa shughuli za umma na maendeleo katika uendeshaji wa Bunge. Hata hivyo, Mfumo wa Kamati za Bunge ulibaki bila mabadiliko.

Ilipofika mwaka 2000, mfumo wa Kamati za Bunge ukafanyiwa mabadiliko kwa kubadilisha Kamati ya Huduma na Haki za Wabunge na kuwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Kamati hii ikachukua jukumu la kuchunguza masuala yote yanayohusu haki, kinga na madaraka ya Bunge pamoja na kushughulikia maadili ya Wabunge, kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni ya 99 (2) ya Kanuni za Bunge, 2000.

Mwaka 2001 mabadiliko mengine yalifanyika kwenye Mfumo wa Kamati za Bunge. Mambo makubwa mawili yalijitokeza kutokana na mabadiliko hayo.

**Kwanza**, iliyokuwa Kamati ya Mashirika ya Umma iliondolewa. Baadhi ya majukumu ya Kamati hiyo yakaweka chini ya Kamati nyingine. Kamati hiyo ni Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma ambayo Kanuni ya 95 (1) (a) ya Kanuni za Bunge, 2001, iliipatia pamoja na mengine, jukumu la kufuatilia hesabu za mashirika ya umma.

> *Kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*
>
> **Siku zisizozidi thelathini na tano kwa ajili ya Bunge kujadili utekelezaji wa bajeti wa kila wizara na taarifa za Kamati za kisekta zililenga kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake**

**Pili**, Kamati nane za Matumizi za Kisekta zilianzishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) na (2) ya Kanuni za Bunge, 2001. Sekta zilizoundiwa Kamati hizo ni sekta ya fedha na uchumi, maendeleo ya Jamii na miundombinu na uzalishaji. Sekta nyingine ni utawala, nje, ulinzi na usalama, biashara na sekta ya huduma za jamii.

Kamati za matumizi za kisekta zilikuwa na masharti tofauti kuhusu uteuzi wa wajumbe, mamlaka ya Kamati na idadi ya siku ya kujadili. Suala la uteuzi wa wajumbe wa Kamati za kisekta, liliwekewa masharti kwenye Kanuni ya 81 (30 ya Kanuni za Bunge, 2001. Kwa masharti hayo, wajumbe waliteuliwa na Spika kutoka miongoni mwa Wabunge na kwamba, kila Msemaji Mkuu wa Upinzani anayehusika na wizara yenye dhamana na sekta, anakuwa mjumbe wa Kamati ya kisekta inayohusika.

Uratibu wa kuzipanga wizara chini ya Kamati za Kisekta, ulimtaka Spika kushauriana na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Mashauriano hayo, yalilenga kumwezesha Spika kupanga wizara ambazo zitashughulikiwa na kila kamati ya kisekta kwa namna yenye tija.

Kamati iliyoshughulikia makadirio ya matumizi kwa fungu au mafungu chini ya wizara inayohusika, haikuwa na malaka ya kufanya mabadiliko katika fungu lolote lililopelekwa kwake kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Mamlaka yake kuhusu mabadiliko, yalikuwa ni ushauri. Utaratibu huu ulizingatia mambo mbalimbali ya mgawanyo wa madaraka, nafasi ya Kamati kwenye Shughuli za Bunge na uwezo halisi wa Kamati, Bunge na Serikali.

Kuhusu muda wa kazi za Kamati za Kisekta, Kanuni zilifafanua kwa namna mbili. **Mosi**, ni muda wa Kamati kushughulikia makadirio ya matumizi ya mwaka unaohusika ambao ulitajwa kuwa siku zisizozidi tano.

Kawaida, wakati Kamati za kisekta ziliposhughulikia makadirio ya matumizi, Bunge lilikuwa likiendelea na vipindi vya maswali na majibu tu. Kwa ajili ya matumizi bora ya muda wa vikao, Bunge liliweza kuanza upokea na kujadili taarifa za Kamati yoyote iliyokamilisha kazi kabla ya siku ya tano.

Namna ya pili, ilihusu muda wa siku zisizozidi thelathini na tano kwa ajili ya Bunge kujadili utekelezaji wa bajeti wa kila wizara na taarifa za Kamati za kisekta. Siku hizo zililenga kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ingawa Mwaka 2002 Bunge lilifanya mabadiliko kuhusu utaratibu wake, kwa sehemu kubwa, Mfumo wa Kamati za Bunge ulibaki kama ulivyokuwa mwaka 2001. Mwaka 2003 majukumu ya Kamati za Matumizi za Kisekta yaliwekwa chini ya Kamati za Kudumu za Bunge.

Kwa tathmini ya jumla kuhusu Kamati za Matumizi za Kisekta, Mwaka 2001 na 2002 Bunge lilitoa kipaumbele cha upekee kwenye namna ya Kamati za Bunge kushughulikia bajeti. Namna hiyo ilitofautishwa na usimamizi wa kawaida wa shughuli za umma za kila sekta. Vilevile, Kanuni ziliweka sharti kwamba, Bunge halitashughulikia fungu lolote la matumizi mpaka baada ya Mwenyekiti wa Kamati inayohusika kutoa taarifa ya kukamilisha kazi.

Hayo yote, yaliyoelezwa yanaonesha Mfumo wa Kamati za Bunge la Tanzania na mabadiliko mbalimbali tangu Mwaka 1961 hadi sasa. Aidha, tafsiri ya mfumo wa Kamati za Bunge imeibua mambo makuu kuhusu aina, utaratibu, mamlaka na mpangilio wa Kamati za Bunge katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge. Nukuu za wabobezi, wataalamu na watafiti mashuhuri wa masuala ya Bunge zimeendana na historia iliyoelezwa.

Kuelekea kuhitimisha, mawazo ya Wataalamu na wabobezi, Prof. Drewry, mtafiti wa masuala ya Kibunge na Bwana Erkine May, mtopezi maarufu wa masuala ya kibunge, yameweka muktadha wa ufafanuzi kama ilivyodhihirika. Kwa kudondoa, Mwaka 1961 kulikuwa na Kamati chache na mfumo wake haukuzingatia baadhi ya mambo ya shughuli za umma wala uhusiano kati ya Bunge na mamlaka ya utendaji.

Baadaye mfumo wa Kamati ulianza kuongeza na kuondoa baadhi ya mambo. Mageuzi ya mfumo wa vyama vya siasa nchini nayo yalichangia mabadiliko. Suala la kuwateua wasemaji wakuu wa kambi la upinzani kwenye Kamati fulasni na kuwepo kwa Kamati za vyama lilitokana na mabadiliko ya mfumo wa vyama vya siasa.

Kuhusu Kamati ya Bunge inayoshughulikia Haki za Bunge ilichukua sura tofauti kadiri miaka ilivyopita hadi kuwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Ushughulikiaji wa Bajeti na usimamizi wa fedha za umma ulioanza mwaka 1961, ulipitia mabadiliko mbalimbali hadi mwaka 2003.

Kwa mfano, Kamati ya Hesabu za Serikali ilianza ikiwa moja na baadaye zikawa mbili. Iliongezeka Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Kamati ya Mashirika ya Umma baadaye ilibadilika kuwa Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma. Kadhalika, awali mfumo wa Kamati za Bunge haukuwa na Kamati za Matumizi za Kisekta, lakini Mwaka 2001 zikawepo na baada ya 2002 zikaondolewa.

Katika toleo lijalo, safu hii itaendeleza ufafanuzi ikiwemo kudadavua mabadiliko ya kimfumo kwenye Kamati za Bunge tangu Mwaka 2003 hadi 2025. Ufafanuzi huu unalenga kuwezesha wasomaji kupata muktadha wa umuhimu wa Kamati za Bunge katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge kulingana na mabadiliko nchini, katika kanda na duniani.

Nasaha za kuhitimisha katika toleo hili ni msisitizo kwamba, ni vema msomaji asikose toleo lijalo, hususani safu hii. Inakumbushwa kwamba "**MWISHO SI MWISHO WA KILA KITU, BALI NI MWANZO WA KITU KIPYA**'.

# Makatibu wa Mabunge ya A. Mashariki wana wajibu wa kufanikisha Jumuiya isiyo na mipaka - *Katibu wa Bunge la Tanzania*



**Katibu wa Bunge Tanzania, Ndg. Baraka Leonard akizungumza wakati wa Kikao cha Makatibu wa Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kilichofanyika Jijini Dar es Salaam**

Na**. Mwandishi Wetu**

Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndg. Baraka Leonard amesema Makatibu wa Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wana wajibu wa kusaidia katika kuendeleza ndoto za waasisi wa Jumuiya hiyo ya kuwa na ustawi endelevu usio na mipaka.

Aliyasema hayo wakati wa Mkutano wa Makatibu wa Mabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Mei 21 hadi 22, 2025 Jijini Dar es Salaam.

Miongoni mwa Makatibu walioshiriki katika kikao hicho ni Naibu Katibu wa Bunge la Kenya, Ndg. Jeremiah Ndombi, Katibu wa Bunge la Somalia, Ndg. Abdirahman Mohamed Abdule na Katibu wa Bunge la Seneti la Kenya, Ndg. Eunice Gichangi.

Wengine ni Naibu Katibu wa Bunge la Uganda, Ndg. Ikior Semakula, Katibu wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Ndg. Alex Lumumba Obatre na Mwakilishi wa Katibu wa Bunge la Rwanda, Ndg. Yankurije Tharcien.

Alisema Waasisi wa Jumuiya hiyo walikubaliana kuwa na maono ya pamoja ya kuiona Afrika Mashariki kama eneo lisilo na mipaka kwa ustawi endelevu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. "Ndoto yao ilikuwa Watu Wamoja. Hatima Moja," alisema.

Katibu wa Bunge alieleza kuwa ndoto ya kuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki ilianza zamani wakati wa jitihada za kihistoria za kuunganisha nchi zetu kwa misingi ya undugu, biashara, utengamano na mshikamano wa kijamii na kisiasa.


"Leo hii, ndoto hiyo imepata sura mpya kupitia mchakato wa ushirikiano wa kisekta, muunganiko wa kifedha, sera za pamoja na hata matarajio ya shirikisho la kisiasa," alisema

Katika hatua nyingine, aliwakumbusha Makatibu wenzake kuwa ni lazima watoke katika hatua ya ndoto na kufikia hatua ya uhalisia kwa vitendo.

"Hali halisi ambapo wananchi wa Afrika Mashariki watahisi, wataona na kunufaika na matunda ya ushirikiano wa Jumuiya," alisema.

Aliongeza kuwa, Waasisi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hawakuwa tu viongozi wa kisiasa bali walikuwa watu wa maono waliotambua kuwa umoja ni hitaji la kisiasa.

"Walielewa kuwa ushirikiano wa kikanda ndio njia pekee ya kuleta amani, maendeleo endelevu na kuinua hali ya maisha ya watu," alisema.



Katibu wa Bunge  la Tanzania, Ndg. **Baraka Leonard** (wanne kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Makatibu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mara baada ya Kikao chao kilichofanyika Jijini Dar es Salaam

> Makatibu wa Mabunge ya Jumuiya hiyo wanapaswa kuhakikisha kuwa mikataba na itifaki za Jumuiya ya Afrika Mashariki inapitishwa kikamilifu kupitia michakato ya kibunge ili kutekeleza kwa dhati dhima ya Waasisi wa Jumuiya hiyo
>
> Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndg. Baraka Leonard

Alieleza kuwa waasisi walijenga dira ya taasisi imara, mifumo thabiti iliyokusudiwa kudumu kwa vizazi.

"Makatibu wa Mabunge ni walezi wa mifumo ya kibunge inayopaswa kuhuisha maono ya waasisi na  kwamba, kazi yao si tu kuyakumbuka maono ya kuanzisha Jumuiya, bali kuyatekeleza kwa vitendo," alisisitiza.

Katibu wa Bunge alisema Makatibu wa Mabunge ya Jumuiya hiyo wanapaswa kuhakikisha kuwa mikataba na itifaki za Jumuiya ya Afrika Mashariki inapitishwa kikamilifu kupitia michakato ya kibunge ili kutekeleza kwa dhati dhima ya Waasisi wa Jumuiya hiyo

Alisema jambo lingine ambalo wanapaswa kulifanyia kazi ni kushirikiana  kimfumo kati ya Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuimarisha mshikamano wa kikanda.

Jambo lingine  ambalo alisema ni muhimu katika kufikia dhima ya kuwa na Jumuiya  ya Watu Wamoja na Hatima Moja ni kuwa na kumbukumbu za kihistoria zilizounda safari ya mshikamano ndani ya jumuiya ili kuwe na mwendelezo kwa vizazi vijavyo.

Sambamba na hayo alisema ni muhimu pia pakawepo na utaratibu wa kuwa na mafunzo ya kuwajengea uwezo waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Mabunge kuhusu masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili wapate ujuzi na nia ya kusukuma mbele ajenda ya Afrika Mashariki.

Mbali na hayo alisema pia ni muhimu kuijengea uwezo Taasisi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa sekretatieti kwa kuwapatia rasilimali za kutosha ili weweze kusimamia ipasavyo maono ya kuanzisha Jumuiya hiyo.



Katibu wa Bunge la Tanzania, Ndg. **Baraka Leonard** akizungumza na Mwakilishi wa Katibu wa Bunge la Rwanda Ndg. **Yankurije Tharcien** wakati wa Kikao cha Makatibu wa Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kilichofanyika Jijini Dar es Salaam

> **Kwa upande mwingine, Katibu wa Bunge alisema anafahamu changamoto zilizopo katika Jumuiya ambazo haziwezi kupuuzwa kama vile ukosefu wa rasilimali, ucheleweshaji wa kiutendaji, tofauti za kisheria miongoni mwa nchi wanachama na haja ya kuoanisha vipaumbele vya kibunge ambavyo ni vikwazo vikubwa katika kufikia ujumuishaji.**

Kwa upande mwingine, Katibu wa Bunge alisema anafahamu changamoto zilizopo katika Jumuiya ambazo haziwezi kupuuzwa kama vile ukosefu wa rasilimali, ucheleweshaji wa kiutendaji, tofauti za kisheria miongoni mwa nchi wanachama na haja ya kuoanisha vipaumbele vya kibunge ambavyo ni vikwazo vikubwa katika kufikia ujumuishaji.

Hivyo aliwaomba Makatibu wa Mabunge katika Jumuiya hiyo kutumia Mkutano huo kama nafasi muhimu ya kukabiliana na changamoto zilizopo kwa njia ya uwazi na washirikiane kutafuta suluhu kwa vitendo.

Katibu wa Bunge alihitimisha kwa kuwahimiza washiriki wa Mkutano huo kujikita katika mijadala yenye tija ili kuboresha mifumo ya kibunge na kuendeleza dira ya Afrika Mashariki iliyoungana na yenye mafanikio.

# Usimamizi wa Kibunge wa Fedha za Umma



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao

Na: **Athuman Hussein**, *ndc*
a.brambati@bunge.go.tz

Chambilecho wahenga, chongo la samaki halifikii mwelekeo bila mkono wa mvuvi. Kinachokusudiwa hapa ni umuhimu wa msukumo au hatua wanazochukua watu wengine kufanikisha uelewa wa umma kuhusu usimamizi wa kibunge wa fedha za umma. Katika toleo lililopita, safu hii ilimaliza kwa msemo "Usipokosa kuelewa hutakuwa na shaka." Lengo lilikuwa ni ujumbe kwamba, "Mwanga wa ufahamu hufuta giza la shaka."

Maneno hayo yalishajiisha wasomaji wa safu na yakafuatiwa na ufafanuzi kuhusu mchakato wa usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma. Maeleo ya ziada yakatolewa kuhusu lengo la mchakato huo sanjari na udadavuaji wa kategoria mbili za mchakato ulioelezwa. Maelezo ya kina yakatolewa ili kuainisha usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma.

Fauka maelezo hayo, upambanuzi ulitolewa kuonesha usimamizi wa fedha za umma kabla ya matumizi (*ex-ante financial oversight).* Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kanuni ya 116 -118 ya Kanuni za Bunge ni sehemu ya marejeo.

Vilevile, Kanuni ya 121 ya Kanuni za Bunge iliongezea katika ufafanuzi wa kazi za Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali na Muswada wa Sheria ya Fedha. Mwisho ilisisitizwa kuwa "Fedha bila nidhamu ni kama maji kwenye tenga, huisha bila faida.

Mwishilizo huo, unatupa dhana ya uwajibikaji ambayo ni kiini katika usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma. Kwa msingi huo, maelezo zaidi kuhusu mchakato wa usimamizi wa fedha za umma kwenye taratibu za Bunge ni maudhui ya makala kwa toleo hili la kumi. Msomaji unakaribishwa kuendelea na safu hii.

Kama ambavyo iliahidiwa katika Toleo la Tisa, toleo hili linafafanua usimamizi wa kibunge wa fedha za umma baada ya matumzi (Ex-post financial oversight). Usimamizi huu kwenye Kanuni za Bunge, unatajwa wazi katika Sehemu ya Nne ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Katika Sehemu hiyo, zimetajwa Kamati za Kudumu za Bunge zinazohusika sambamba na kuweka wazi majukumu ya Kamati hizo.

Kwa ufafanuzi zaidi, usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma ni mchakato unaohusisha jukumu la Bunge kupitia, kutathmini na kuihoji Serikali (mamlaka ya kiutendaji)



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao

> **Ibara ya 143** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mambo mengine, imempa CAG wajibu wa kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali, hesabu za mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

baada ya kuwa imefanya matumizi ya fedha za umma. Ufafanuzi huo ni mwendelezo wa maelezo kuhusu usimamizi wa fedha za umma kabla ya matumzi (ex-ante financial oversight) yaliyoanza kutolewa katika Toleo la Tisa.

Lengo kuu la usimamizi wa matumizi ya fedha za umma linahitaji kueleweka. Vinginevyo inaweza kushangaza kama si kukanganya kwa msomaji kusoma dhana inayoitwa usimamizi wa fedha baada ya matumizi na kutarajia maelezo ya usimamizi kabla ya maumizi. Ufafanuzi unaofaa utahusishwa na lengo la usimamizi wa fedha za umma kabla ya matumzi (ex-ante financial oversight). Lakini kwa kuanzia, lengo la usimamizi wa matumzi ya fedha za umma kwa hatua ya baada ya matumizi kufanyika (ex-post financial oversight) lieleweke.

Bunge linaposimamia matumizi ya fedha za umma linalenga kuhakikisha kwamba, Serikali inawajibika kwa matumizi yake ya fedha za umma na hatua zake za kisera kuhusu matumizi hayo. Bunge linafanya hivyo kwa madaraka lililonayo ili kugundua, kuzuia na kurekebisha usimamizi mbaya, uzembe na ufisadi unaoweza kufanywa na watendaji au maofisa wakuu Serikalini.

Dhana kuu zinazochomoza katika maelezo hayo ni pamoja na "uwajibikaji" katika matumizi ya fedha za umma, uzembe unaohusu matumizi ya fedha za umma na usimamizi wa fedha za umma serikalini. Ufafanuzi wake

utatolewa kwenye matoleo yajayo ili kutokuvuruga mtirirko wa maelezo kuhusu usimamizi wa matumizi ya fedha za umma unaoendelea katika toleo hili.

Katika dhana ya Bunge kusimamia matumizi ya fedha za umma, kuna mchakato mrefu na mchakato mfupi. Mchakato mrefu unapokea mwishilizo wa hatua ya Bunge kupitia/kujadili makadirio ya mapato na matumizi na kuidhinisha bajeti ya Serikali. Hatua hizo zilielezwa katika toleo lililopita. Kwa ufupi, mchakato huo unaanzia utoaji wa fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali hadi kwa maofisa masuuli ambao wanasimamia matumizi ya fedha za umma ndani ya Serikali. Baadaye ukaguzi wa matumizi hayo hufanyika na ripoti kulifikia Bunge.

Mchakato wa kibunge wa kusimamia matumizi ya fedha za umma baada ya matumizi, unaanzia pale ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, maarufu kwa jina la CAG zinapowekwa mezani Bungeni kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 ya Sheria za Tanzania.

Kwa mfano, itakumbukwa kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania alisema "Sisi upande wa Serikali… tutasikiliza vizuri na kufuatilia vizuri mjadala wa Bunge kwenye Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali." Aliyasema hayo tarehe 28 Machi, 2025 alipokuwa akipokea Taarifa mbili. Miongoni mwa taarifa hizo ni Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2024.

Maneno hayo yanaonesha kuwa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itajadiliwa na Bunge. Kibunge, Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, huingia kwenye mchakato wa kibunge zinapowasilishwa mezani na baadaye Bunge kujadili na kutoa maazimio yake. Utaratibu huo umeelezwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kwa urahisi wa maelezo, mchakato huo unaweza kuelezwa katika hatua saba.

**Mosi**, ni taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilishwa mezani. Yaani kuwekwa mezani Bungeni ambapo wahusika ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na CAG mwenyewe.

Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mambo mengine, imempa CAG wajibu wa kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali, hesabu za mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge. Ibara hiyo pia inamtaka CAG kuwasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa Katiba. Chini ya Ibara hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amepewa jukumu la kuwaagiza watu wanaohusika kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge utakaofanyika mara tu baada ya Rais kupokea taarifa ya CAG.

Kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 ya Sheria za Tanzania kimeweka masharti kwamba, Taarifa za CAG zitawekwa mezani Bungeni na Waziri anayehusika. Nakala ya Taarifa inayopaswa kuwekwa mezani Bungeni, ni ile inayoandaliwa baada ya CAG kutoa matokeo ya mwisho ya ukaguzi na kuzipatia menejimenti za taasisi zenye hesabu zilizokaguliwa na kisha kupokea majibu yanayojulikna kwa jina la "*Management Responses*" ambayo hutolewa ndani ya siku ishirini na moja.

Kanuni ya 43(1) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inamruhusu Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweka mezani jambo linalohusika kwa utaratibu wa hati za kuwasilisha mezani. Madhumuni ya kuwasilisha mezani ni kusajili rasmi Taarifa zinazowasilishwa kwenye mchakato wa kibunge kwa mujibu wa taratibu na desturi za Bunge. Hatua hii inaanzisha rasmi tafakuri za Wabunge kuhusu taarifa hizo. Vilevile ni hatua muhimu inayowezesha upatikanaji wa maoni au ufuatiliaji wa umma kuhusu namna Bunge linavyoshughulikia taarifa hizo.

**Pili**, ni hatua ya kukabidhi taarifa hizo kwa Kamati inayohusika. Mchakato huo unazingatia masharti ya kifungu cha 38 (4) na (5) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma kinachoonesha kwamba, Bunge litajadili taarifa ya CAG baada ya Kamati za Kusimamia Matumizi ya Fedha za Umma kukamilisha kazi.

Kwa msingi huo, hatua ya kuzikabidhi Kamati zinazohusika Taarifa ya CAG, ni jambo linalowezesha uzingatiaji wa Sheria. Hatua hii pia ipo ndani ya wigo wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni ya 43(8) ya Kanuni za Bunge inataka Taarifa zinazowekwa mezani Bungeni zijadiliwe na Kamati zinazohusika.

Tafsiri ya Kamati inayohisika imetolewa na Kanuni ya 136(14) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hiyo, Kamati inayohusika ni Kamati yoyote ambayo Spika ataipelekea Muswada wa Sheria au jambo lingine lolote. Pamoja na tafsiri hiyo, kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, Kamati zinazohusika na Taarifa ya CAG ni Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma.

Kamati hizo zimetajwa katika Sehemu ya Nne ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kifungu cha 12 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimezitaja Kamati mbili: Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, maarufu PAC na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, maarufu LAAC.

**Tatu**, ni Kamati kuwasikiliza maofisa masuuli. Watu wengine huiita hatua hii kwa kiingereza kuwa ni "Committee hearing". Lengo la kuwasikiliza maofisa masuuli ni kuhakikisha kuwa wanawajibika kwa matumizi ya fedha za umma kwa kutoa maelezo kuhusu hoja mbalimbali zitokanazo na ukaguzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 9 cha Sheria ya Fedha za Umma, ofisa masuuli anao wajibu wa kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Kifungu hicho kinaonesha pia kuwa maofisa masuuli wanawajibika kwa matumizi ya fedha za umma. Matumizi hayo yanatarajiwa kufanyika kulingana na Sheria ya Fedha za Matumzi ya Serikali. Yaani, *The Appropriation Act*.

Ofisa masuuli ndiye mwenye dhamana ya usimamizi wa fedha katika taasisi au wizara, hivyo anatakiwa kueleza namna fedha za umma zilivyotumika. Anapoitwa na Kamati anatakiwa kujibu hoja zilizoibuliwa. Mara nyingi CAG huibua hoja za ukiukwaji wa taratibu na ubadhirifu wa na matumizi yasiyo na ufanisi. Kwenye Kamati zinazosimamia matumizi ya Fedha za Umma, maofisa masuuli huitwa na kusikilizwa wanavyotoa maelezo na majibu kuhusu masuala hayo.

Vilevile, maofisa masuuli husikilizwa ili kupata maelezo ya ufafanuzi au uthibitisho wao kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya CAG au ya Bunge juu ya udhibiti wa fedha za umma. Kwa nafasi zao, wanapaswa kuwajibika kwa wananchi kupitia Bunge ambalo ni chombo cha wawakilishi wao.

Kinachotakiwa ni maofisa hao kuipatia Kamati inayohusika maelezo sahihi na ya kina juu ya utendaji wa taasisi zao kuhusiana na matumizi ya fedha za umma. Kwa ujumla, kuwaita maofisa masuuli kwenye Kamati ni sehemu ya mfumo wa uwajibikaji na usimamizi wa fedha za umma kwa lengo la kuhakikisha uwazi, nidhamu ya matumizi na utawala bora.

Pamoja na kuwasikiliza au kuwahoji maofisa masuuli, Kamati hutumia utaratibu wa kupokea maoni ya wataalamu (*expert opinion*) na ikibidi wadau wengine. Jambo hili limetambuliwa na kuruhusiwa na Kanuni za Bunge. Kanuni ya 136(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeruhusu Kamati za Kudumu za Bunge kujiwekea utaratibu wa kutekeleza majukumu yake alimradi usiwe unaathiri masharti mengine ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Utaratibu huo unawezesha Kamati kupata maoni ya wataalamu na uelewa wa kina kuhusu hoja zinazoshughulikiwa

Vilevile, Kamati zimeruhusiwa kualika Wabunge wengine au watu ambao si Wabunge kuhudhuria na kushiriki katika shughuli za Kamati bila kuwa na haki ya kupiga kura. Masharti hayo ya Kanuni ya 136(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, yanatumika wakati Kamati inapowasikiliza maofisa masuuli kwa utaratibu maalumu. Utaratibu huo unawaondoa watu wasio wajumbe kwenye hatua za mwisho za kujenga msimamo wa Kamati. Hata hivyo kwa wakati huo, Kamati inakuwa imekwishapata undani, maoni ya watu wengine wakiwemo wataalamu na majibu ya maofisa masuuli.

Utaratibu unaotumika, unawezesha Kamati kuanza kwa kupokea vidokezo vya Sekretarieti na maoni ya wataalamu mahsusi. Hatua hizo hufuatiwa na Wajumbe kujipanga kimwelekeo kwa ajili ya mahojiano na maofisa masuuli. Baada ya hivyo, maofisa masuuli huhojiwa na majibu kurekodiwa kwa ajili ya uchanganuzi na uchambuzi.

Uamuzi wa Kamati unaojenga msimamo utokanao na hayo, hufanyika kwa kuzingatia maoni ya wajumbe waliowengi. Masharti kuhusu uamuzi wa Kamati yamefafanuliwa kwenye Kanuni ya 136(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hiyo inataka maoni ya Kamati yawe ni maoni ambayo yamekubaliwa na wajumbe walio wengi. Kwa maneno mengine, hiyo ni dhana ya wengi wape inayoitwa kwa lugha nyingine "majority rule".

**Nne**, ni Kamati kutoa taarifa yake Bungeni. Kifungu cha 38(4) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, kinaweka sharti kwamba, Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma zitakapokamilisha kazi ya kupokea maoni, maelezo na kujadiliana, ziandae taarifa na kuwasilisha Bungeni zikiwa na maelezo na mapendekezo.

Kwa masharti hayo, Taarifa za Kamati zinapaswa kuelezea hoja zilizoibuliwa na CAG, majibu na tathmini ya majibu hayo sanjari na kubainisha maoni na mapendekezo. Mantiki ya maudhui ya kifungu cha 38 (4) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, inajengwa kwenye umuhimu wa Bunge kupata maelezo yaliyochakatwa kuhusu matokeo ya ukaguzi na majibu ya maofisa masuuli.

Katika desturi za Bunge la Tanzania, Taarifa za Kamati huingia Bungeni kwa utaratibu unaotambuliwa chini ya Kanuni ya 36(4) (m) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa Kanuni hiyo, Taarifa huingia Bungeni zikiwa ni hoja za Kamati. Kwa mantiki hiyo, masharti kuhusu hoja chini ya Kanuni za Bunge hutumika. Kwa mfano, Kanuni ya 61(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge hutumika na kuzifanya Taarifa hizo ziwe na mapendekezo ya Maazimio kwa mfumo wa maneno unaojumuisha maneno: **"Bunge limeazimia kwamba…"**

**Tano** ni mjadala wa Bunge kuhusu Taarifa ya CAG kupitia Taarifa za Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma. Kifungu cha 38(5) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma kinaelekeza kwamba, Taarifa za Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma kutokana na Taarifa za CAG, zijadiliwe kwa pamoja na Taarifa jumuifu ya majibu na mpangokazi wa kushughulikia hoja za CAG zitakazowasilishwa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Kifungu cha 38(2) cha Sheria hiyo, kinataka iandaliwe Taarifa Jumuifu ya majibu na Mpango wa kutekeleza mapendekezo ya CAG. Kwa mujibu wa Kifungu cha 38(3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma,Taarifa hiyo inapaswa kuwasilishwa mbele ya Bunge katika Mkutano wa Pili baada ya Mkutano ambao Taarifa ya CAG iliwekwa mezani. Kifungu cha 38(1) kinazitaka Kamati zinazosimamia matumizi ya Fedha za Umma kufanyia kazi Taarifa ya CAG kwa pamoja na Taarifa Jumuifu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Bunge linapokuwa likijadili Taarifa ya Kamati, marejeo ni Taarifa ya CAG. Jambo hili linaanzia kwenye Kamati hizo. Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeifunga kazi ya Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma kwenye Taarifa za CAG. Kwa msingi huo, taarifa za Kamati kuhusu matumizi ya fedha za umma zinatokana na Taarifa za CAG.

Kadhalika, Kanuni ya 67(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inawataka wachangiaji wakati wa mjadala Bungeni kuzungumzia jambo ambalo liko kwenye mjadala. Kwa maana hiyo, Kanuni zinataka wanaojadili wajielekeze kwenye hoja inayotokana na Taarifa za CAG.

Uamuzi wa Bunge unapatikana kwa kuongozwa na mapendekezo ya Kamati ambayo ni Rasimu ya Maazimio ya Bunge kama ilivyofafanuliwa kwa kurejea Kanuni ya 61(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Wakati wa mjadala, hoja hutolewa Bungeni ili iamuliwe. Uamuzi huo unaweza kufanyika kwa kuzingatia au kutokuzingatia mapendekezo yanayotolewa kuhusu hoja. Mjadala utaelekea kwenye mambo matatu yanayotokana na masharti ya Kanuni ya 64 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Jambo la kwanza ni kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine. La pili ni kuondoa maneno fulani bila kuingiza maneno mengine. Na la tatu ni kuingiza au kuongeza maneno mapya kwenye hoja. Ikumbukwe kuwa hoja ya Kamati kuhusu Taarifa za CAG itakuwa katika muundo wenye maneno **"Bunge linaazimia kwamba…".**

Kwa maana hiyo, namna tatu zilizoelezwa kuhusu hoja zinahusu maneno yanayofuata baada ya kifungu cha maneno "**Bunge linaazimia kwamba…"** ambayo ndiyo hasa uamuzi wa Bunge. Kwa hiyo utaratibu huo unalenga kupata uamuzi wa Bunge ulio bayana unaowekwa kwa lugha ya moja kwa moja.

Muhimu zaidi imesisitizwa kwamba, kila badiliko linalopendekezwa, sharti liwiane na hoja inayokusudiwa. Masharti kuhusu pendekezo la mabadiliko ni pamoja na kutokuingiza jambo ambalo kwa maoni ya Spika linaweza kuwasilishwa kwa hoja maalumu. Masharti hayo yanazatiti utaratibu wa kushughulikia Taarifa za CAG na kupata uamuzi wa Bunge kwa muundo wa Maazimio ya Bunge.

**Sita**, ni Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Hatua hii inaliwezesha Bunge kupata mrejesho juu ya utekelezaji wa maazimio yake yaliyotokana na Taarifa za CAG. Mabunge mengi duniani yana changamoto kuhusu upatikanaji wa mrejesho juu ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge yanayotokana na Taarifa za Ukaguzi.

Bunge la Tanzania hivi karibuni limepiga hatua ya kuweka utaratibu madhubuti wa kupokea mrejesho wa utekelezaji. Kwa desturi, Taarifa za Kamati hujadiliwa mwezi Oktoba au Novemba kila Mwaka. Taarifa ya utekelezaji hutolewa kwa Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za Umma. Kamati hizo hufanya ulinganisho baina ya taarifa ya utekelezaji iliyowekwa

Mezani Bungeni na maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa za Kamati hizo.

Kwa kujumuisha, safu hii katika Toleo la Kumi imefafanua mchakato wa usimamizi wa kibunge wa fedha za umma, katika hatua baada ya matumizi (*ex-post financial oversight*). Kwa ujumla imefanya mwendelezo wa maudhui ya toleo lililopita ambalo lilieleza usimamizi wa fedha za umma kabla ya matumizi (*ex-ante financial oversight*).

Hatua saba za usimamizi huo wa kibunge zimeelezwa kwa kurejea Sheria kuu inayohusika pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge. Hatua hizo ni: uwasilishaji wa taarifa ya CAG Bungeni, kukabidhi taarifa kwa Kamati zinazohusika na Kamati kuwahoji maofisa masuuli. Hatua nyingine ni Kamati kuwasilisha taarifa Bungeni, mjadala wa Bunge, ufuatiliaji wa Maazimio ya Bunge na ripoti ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuwekwa Mezani na Kamati zinazohusika.

Kwa kuhitimisha, usimamizi wa kibunge wa fedha za umma baada ya matumizi ni nguzo muhimu katika kuhakikisha uwajibikaji, ufanisi na matumizi yenye tija ya rasilimali za taifa. Bunge linatumia mamlaka yake kufuatilia na kuhoji matumizi ya fedha ili kuzuia uzembe na ufisadi. Mfumo huo wa ufuatiliaji hutoa fursa kwa wananchi, kupitia kwa wawakilishi wao, kuhakikisha kwamba, Serikali inatekeleza majukumu yake kwa uwazi na kwa kufuata taratibu.

Mwishilizo huo, unaalika ufafanuzi kuhusu dhana ya uwajibikaji ambayo ni msingi wa utawala bora na maendeleo ya kweli ya taifa. Kwa sababu hiyo, safu hii katika Toleo lijalo, itaelezea dhana ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ikiwa ni sehemu muhimu ya utawala bora kwenye matumizi ya fedha za umma. Kubwa la kukumbuka ni kuwa misingi ya uwajibikaji haipaswi tu kuwekwa, bali inapaswa kuzingatiwa, kuchunguzwa kwa umakini na kuhojiwa, maana humo ndimo ulipo moyo wa uhakika wake. SHIME, MSOMAJI MWENYE KIU YA KUELEWA KWA UNDANI ZAIDI.







# Bunge la 12 larekebisha Kanuni za Kudumu za Bunge



Naibu Spika wa Bunge, Mhe. **Mussa Azzan Zungu** akizungumza Bungeni

Na. **Christina Nkya**

Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Kikao chake cha 44 cha Mkutano wa 19 wa Bunge kilichofanyika tarehe 11 Juni, 2025 lilirekebisha Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.

Marekebisho hayo yalipitishwa na Waheshimiwa Wabunge mara baada ya Naibu Spika wa Bunge na ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kuwasilisha taarifa ya Kamati hiyo kuhusu Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni hizo.

Akiwasilisha taarifa hiyo, Mheshimiwa Zungu alisema kwa kuwa Bunge la 12 linaelekea mwisho wa kipindi cha uhai wake, imeonekana ni muhimu kuzipitia Kanuni hizo kwa lengo la kuziboresha ili zitumike wakati wa Bunge la Kumi na Tatu litakaloanza Novemba, 2025.

"Utaratibu huu ni wa kibunge na huzingatiwa na mabunge mengine ya Jumuiya za Madola," alisema.

Alisema wakati wa kufanya marekebisho hayo Kamati ilibaini uwepo wa maeneo mbalimbali katika Kanuni yenye changamoto zinazohitaji kupatiwa ufumbuzi wa kanuni.

Aliainisha kuwa moja ya maeneo hayo ni kuhusu uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge na Wajumbe wa Tume ambapo Kamati ilibaini kuwa katika Kanuni zilizopo haujabainishwa utaratibu katika Kanuni unaosimamia uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge na Wajumbe wa Tume katika mazingira ambayo idadi ya majina ya wagombea inalingana na nafasi zilizopo.

> Kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati za Bunge hutakiwa kuwasilisha Taarifa za Kamati wakati wa Mkutano wa Bunge wa Mwezi Januari-Februari.
>
> Naibu Spika wa Bunge na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni, Mhe. **Mussa Azzan Zungu**

Aidha alisema utaratibu wa kupiga kura unaotakwa katika Kanuni ya 92 ya Kanuni za Kudumu za Bunge umekuwa unatumika unaozingatia uamuzi wa Bunge unaotokana na Spika hulihoji Bunge ambapo Wabunge huitikia kwa pamoja kwa sauti za wanaafiki au wasioafiki.

Hivyo alisema Kamati imependekeza kufanya marekebisho ya kanuni ili kuweka masharti yatakayowezesha uchaguzi wa Wenyeviti katika mazingira hayo.



> "Hivyo, inapendekezwa tuweke utaratibu huo katika Kanuni ambapo Wabunge watatoa ahadi ya uadilifu katika kila Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge ambapo kila Mbunge ataahidi kuwa mtiifu na mwaminifu kwa nchi yetu na kufanya kazi zake kwa uadilifu," alisema.

Jambo lingine ambalo alisema Kamati iliona ni vyema kuliongeza kwenye Kanuni za Bunge ni ahadi ya uzalendo.

Alisema baadhi ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola yanao utaratibu wa Wabunge kutoa ahadi ya uzalendo katika vikao vyake.

"Hivyo, inapendekezwa tuweke utaratibu huo katika Kanuni ambapo Wabunge watatoa ahadi ya uadilifu katika kila Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge ambapo kila Mbunge ataahidi kuwa mtiifu na mwaminifu kwa nchi yetu na kufanya kazi zake kwa uadilifu," alisema.

Aliongeza kuwa ahadi hiyo humaanisha kuwa, Wabunge watakuwa wazalendo wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kibunge.

Pia alisema suala lingine ambalo kanuni za sasa hazijaweka utaratibu unaoeleweka ni wa kupiga kura kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kutumia neno abstain wakati wa kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali.

Alisema kutokana na kutotambulika katika kanuni kwa kura hiyo, imekuwa ni changamoto katika uwekaji wa taarifa za zoezi la kupiga kura.

"Hivyo, inapendekezwa suala hili lisimamiwe katika Kanuni ili kurekodi kura hiyo ya abstain. Vilevile inapendekezwa kuitambua kura hiyo kwa maneno Sipigi Kura ambayo ni tafsiri ya neno hilo katika lugha ya Kiswahili,"alisema.

Suala lingine ambalo alisema Kamati iliona inafaa liwekwe kwenye Kanuni ni muda wa Kusoma Bajeti Kuu ya Serikali.

Alisema uzoefu umeonesha kuwa Bajeti Kuu ya Serikali imekuwa ikisomwa saa 10:00 jioni lakini muda wa kusoma Bajeti haupo katika kanuni ya 124 inayosimamia suala hilo.

"Kamati inapendekeza yafanyike marekebisho ili kutambua muda wa kusoma Bajeti ya Serikali kwamba itakuwa ni saa 10:00 jioni lakini vilevilie kuwezesha kuendana na makubaliano ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kusoma

Bajeti zao Kuu za Serikali kwa pamoja wakati huo," alisema.

Jambo lingine ambalo alisema limeongezwa kupitia marekebisho hayo ni Mkutano unaoitishwa na Spika kujadiliana na Wabunge kuhusu masuala ya kibunge ambao haujatajwa katika kanuni za sasa, hivyo ilipendekeza Mkutano huo utambuliwe rasmi na Kanuni.

Akizungumza kuhusu Taarifa za Kamati za Hesabu na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Naibu Spika alisema kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati za Bunge hutakiwa kuwasilisha Taarifa za Kamati wakati wa Mkutano wa Bunge wa mwezi Januari-Februari.

Aliongeza kuwa Bunge linao utaratibu wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma huwasilisha Taarifa za Mwaka katika Mkutano wa mwezi Oktoba-Novemba.

"Utaratibu huo haujawekwa katika Kanuni. Kutokana na umuhimu katika kusimamia fedha na mitaji ya umma, Kamati inapendekeza utaratibu huo wa kuwasilisha Taarifa uwekwe katika Kanuni," alisema.

Kuhusu suala la Utambulisho wa Wageni Bungeni, alisema Kanuni za Bunge zimeweka utaratibu wa kutambulisha wageni Bungeni lakini utambulishaji wa wageni umeonekana kuchukua muda mwingi wa Bunge jambo hilo linalopunguza muda uliotengwa kwa Shughuli za Bunge.

Kwa sababu hiyo alisema Kamati inapendekeza kufanya marekebisho ya kanuni ya 161 kwa lengo la kuokoa muda wa Shughuli za Bunge kwa kutambulisha wageni mahususi wa kitaifa na kimataifa waliopo katika Ukumbi wa Bunge pamoja na wageni waliotoa mchango wa kitaifa unaohitaji kuenziwa.

Kuhusu suala la upeperushaji wa Bendera ya Bunge, Naibu Spika alisema Wabunge wanaruhisiwa kupeperusha Bendera ya Bunge katika ofisi zao na katika magari yao binafsi lakini hata hivyo Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya matumizi yasiyo sahihi ya Bendera yanayosababisha kushusha hadhi na heshima ya Mbunge.

Hivyo, alisema Kamati inapendekeza kuweka masharti ya kusimamia upeperushaji wa Bendera katika gari la Mbunge.

Alisema mapendekezo hayo ni ya kumzuia Mbunge kupeperusha Bendera akiwa anaendesha gari lake, Mbunge kutopeperusha katika gari lake Bendera zaidi ya moja kwa wakati mmoja na vilevile kuelekeza kuwa Mbunge anapaswa kupeperusha bendera akiwa ameketi upande wa kushoto wa gari lake likiwa linaendeshwa na Dereva.

Marekebisho mengine ambayo Naibu Spika aliyazungumzia ni utaratibu wakati wa kuridhia mkataba wa kimataifa ambapo alisema Kanuni ya 110 imeweka utaratibu wa Bunge kujadili na kupitisha Azimio kuridhia au kutoridhia mkataba wa kimataifa.

Aliongeza kuwa utaratibu huo umeeleza jinsi hoja itakavyowasilishwa na Msemaji wa Serikali bila kueleza nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Bunge iliyofanya uchambuzi na vilevile Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni.

Hivyo alisema Kamati imependekeza kuongezwa kwa kanuni ndogo mpya katika kanuni ya 110 inayoweka sharti kwa Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Mkataba pamoja na Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni kutoa maoni yao kabla ya Wabunge kujadili na kufanya uamuzi kuhusu Mkataba husika.

Kuhusu kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais, alisema mapendekezo ni kuwa na kanuni mahsusi inayoeleza utaratibu wa Bunge wa kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais pale inapotokea ameteuliwa baada ya kipindi cha uchaguzi kupita (Ibara ya 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977).

> **Inapendekezwa kuweka Kanuni inayokataza mavazi hayo ili kudumisha dhana ya Bunge kuendesha shughuli zake kwa uhuru na umoja bila kujali itikadi za kisiasa. Aidha, Kanuni kuhusu mavazi imeboreshwa ili kuweka usimamizi madhubuti wa mavazi Bungeni**

"Utaratibu unaopendekezwa unatokana na uzoefu wa Bunge letu kuendesha mchakato kama huo," alisema.


Miongoni mwa jambo lingine ambalo Naibu Spika alisema limefanyiwa marekebisho ni suala la mavazi hususan kwa Waheshimiwa Wabunge baada ya kubainika kuwa baadhi ya wanaoingia maeneo ya Bunge huvaa sare zinazoshiria au kuzoeleka kuvaliwa na wafuasi au mashabiki wa vyama vya siasa kwa alama, nembo, maandishi ambavyo hutafsiriwa kwa jina, alama, msemo au nembo ya chama.

"Inapendekezwa kuweka Kanuni inayokataza mavazi hayo ili kudumisha dhana ya Bunge kuendesha shughuli zake kwa uhuru na umoja bila kujali itikadi za kisiasa. Aidha, Kanuni kuhusu mavazi imeboreshwa ili kuweka usimamizi madhubuti wa mavazi Bungeni," alisema.

Kwa upande mwingine baada ya Naibu Spika kuwasilisha taarifa hiyo kuhusu marekebisho hayo ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kuzijadili na kutoa maoni yao kabla ya kupitisha.

Akizungumza mara baada ya Waheshimiwa Wabunge kuridhia marekebisho hayo, Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson alisema kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria Kanuni hizo zitachapishwa katika Gazeti la Serikali na kisha zitaanza kutumika Bunge lijalo la 13.

# Misingi ya Utaratibu na Uendeshaji wa Bunge



Spika wa Bunge Mhe. Dkt **Tulia Ackson** akimpisha Naibu Spika wa Bunge, Mhe. **Mussa Azzan Zungu** kuongoza Kikao cha Bunge

Na: **Athuman Hussein,** *ndc*
a.brambati@bunge.go.tz

Katika toleo lililopita, maelezo kuhusu misingi ya utaratibu na uendeshaji wa Bunge yalihusu ufafanuzi wa hoja ndogo. Ufafanuzi huo ulipokea mwishilizo wa toleo la nane lililofafanua dhana ya hoja na aina zake kwa muktadha wa Bunge.

Msingi na umuhimu wa maelezo hayo ni ukweli kwamba, uendeshaji wa Bunge unafuata mfumo wa utaratibu wa kibunge unaotaka hoja itolewe, iungwe mkono, ijadiliwe, ihitimishwe na kisha iamuliwe. Kwa mfumo huo, ni vigumu kufuatilia inavyostahili uendeshaji wa vikao vya Bunge bila kuelewa dhana ya hoja.

Katika toleo hili, ushawishi wa nadharia ya "maendeleo ya maarifa" ambayo inachanganya mawazo ya wanafalsafa John Dewey (Mwanafalsafa wa Kimarekani) na Aristotle (Mwanafalsafa wa Kigiriki), unaisukuma safu hii kuendeleza maelezo ya hoja. Wanafalsafa hao kwa pamoja, wanaamini kuwa maarifa si tukio la mara moja, bali ni safari endelevu.

Mtazamo huo unaaminisha kuwa "uelewa kuhusu hoja utapatikana kwa kuendelea kusoma na kufuatilia ufafanuzi unaoendelea kuhusu jambo hili linaloguswa katika misingi ya utaratibu na uendeshaji wa Bunge. Kwa msomaji aliyepitia matoleo yaliyopita hususan safu hii, atabaini kuwa alipata maelezo kuhusu hoja kuu, hoja ndogo na hoja zenye hadhi maalumu.

Mifano fafanuzi na halisi ilitolewa kwa aina mbili za hoja. Aina hizo ni hoja kuu na hoja ndogo. Toleo hili linakusudia kufafanua hoja zenye hadhi maalumu.

Kwa tafsiri, hoja zenye hadhi maalumu ni mapendekezo yanayotolewa Bungeni ili yajadiliwe na kuamuliwa. Mapendekezo hayo yanastahili upendeleo katika mfuatano wa shughuli za vikao vya Bunge. Sababu za kupewa kipaumbele ni umuhimu wake kutokana na athari zake kwenye utaratibu wa Bunge. Mahitaji ya hadhi maalumu kwa hoja hizo, yanatokana na sababu tatu.

**Kwanza,** ni umuhimu wa kujenga imani ya Bunge kwa umma. Kwa kuwa asili ya hoja zenye hadhi maalumu inataka zifanyiwe kazi mapema, uamuzi wa Bunge unapatikana mapema. Mchakato huo unapohusu hoja zenye kugusa maslahi ya umma na uimara wa misingi ya demokrasia, inachangia kuuwezesha umma kuliamini Bunge.

Hoja zinazohusu haki za Bunge, zinahusu ukiukaji au uvunjifu wa haki za Bunge. Hoja hizo ni mapendekezo yanayolotolewa Bungeni ili kushughulikia masuala ya haki za Bunge. Kuifafanua vizuri aina hii ya hoja, kuna umuhimu wa kukumbuka fasili ya dhana "**haki za Bunge**".



**Pili,** ufanisi wa Bunge na uwakilishi Bungeni unategemea haki maalumu za Wabunge katika kutekeleza majukumu yao. Kutokuwa na kipaumbele kwa hoja zinazohusu haki na hadhi kwa nafasi zao za uwakilishi, si rahisi kwa Mbunge mmoja mmoja kuwa na uwakilishi unaofaa.

**Tatu**, mwenendo wa vikao vya Bunge unagusa usimamizi wa maslahi ya wananchi. Ili mwenendo huo uwe na tija kwa umma, lazima kuwe na kinga. Pasipo kinga kwa mwenendo na utaratibu, uhuru wa chombo chenyewe utakuwa hatarini.

Hoja zinazohusu haki za Bunge, zinahusu ukiukaji au uvunjifu wa haki za Bunge. Hoja hizo ni mapendekezo yanayolotolewa Bungeni ili kushughulikia masuala ya haki za Bunge. Kuifafanua vizuri aina hii ya hoja, kuna umuhimu wa kukumbuka fasili ya dhana "**haki za Bunge**".

Nguli wa masuala ya kibunge, bwana Erskine May, alifasili "**haki za Bunge**" kuwa "ni jumla ya haki za kipekee za kila Bunge kwa pamoja na za Mbunge mmoja mmoja, ambazo bila kuwa nazo, Mabunge na Wabunge hawataweza kufanya kazi yao na kwamba, haki hizo zinazidi haki ambazo vyombo vingine au watu wengine wanazo."

Naye Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa zamani, Mheshimiwa Andrew John Chenge, aliwahi kuwaeleza Wabunge kwamba, "Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge" inajumuisha haki za kuendesha shughuli za Bunge na Kamati zake." Aliyasema hayo tarehe 26 Januari 1996, katika semina ya Wabunge wote. Maelezo yake hayakukinzana na fasili ya Haki za Bunge iliyoelezwa awali.

Ufafanuzi wote huo unajenga muktadha wa hoja kuhusu masuala ya haki za utendaji wa Bunge au Kamati zake. Kwa sababu hiyo, hoja yoyote inayogusa utatuzi wa suala la haki za kipekee kuhusu utendaji wa Bunge au Kamati zake, inahitaji kupewa kipaumbele zaidi ya hoja za kawaida. Kwa kuzingatia fasili ya Haki za Bunge na maelezo ya Mheshimiwa Chenge, inafaa kuona na kukubali kwamba, hoja kuhusu masuala ya haki za Bunge inaweza kugusa mambo makuu manne.

**Moja**, ni haki kuhusu Bunge kama taasisi. Kwa suala hili, hoja inayotolewa Bungeni, inaweza kuhusu haki za Bunge kwa sura ya taasisi. Katika pendekezo au hoja hiyo, jambo kuu hulenga kuhakikisha uhuru wa Bunge na utendaji wake.

Kwa mfano, katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge anaweza kutoa hoja kuhusu haki za Bunge iwapo ataona kuwa matamko ya viongozi wa Serikali au vyombo vya dola ni uvunjifu wa haki za Bunge kama taasisi. Hoja ya aina hiyo ni miongoni mwa hoja zenye hadhi maalumu zinazostahili kupewa kipaumbele katika mpangilio wa hoja zinazofanyiwa kazi na Bunge.

**Mbili**, ni haki za Mbunge mmoja mmoja. Kwa muktadha huo, hoja inayotolewa inaweza kulenga haki za Mbunge mmoja mmoja ambazo ni maalumu kwa Mbunge. Haki hizo zinalenga kumlinda Mbunge aweze kutekeleza majukumu yake. Hoja kama hiyo ina hadhi maalumu na inastahili kupewa kipaumbele kuliko hoja za kawaida.

Mantiki hasa ni kwamba, mijadala katika hoja za aina yoyote itakuwa na tija iwapo Mbunge mmoja mmoja atakuwa huru na ataona kuwa yupo huru kutoa maoni yake. Itawezekana kuwa hivyo, iwapo hoja inayohusu haki maalumu na za kipekee kwa Wabunge zitapewa kipaumbele na upendeleo maalumu.

**Tatu**, ni haki za utendaji wa Kamati ya Bunge. Ili kupata tija ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati za Bunge, unahitajika uhuru katika utaratibu wa uendeshaji wake na ufanyaji kazi wa Wajumbe wake. Bunge ambalo linategemea ufanisi wa Kamati zake, linapaswa kutoa kipaumbele kwa hoja yoyote inayogusa ukiukaji wa haki za Bunge kwenye Kamati za Bunge.

Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Februari, 2023 zinafafanua namna hoja zinazohusu masuala ya haki za Bunge zinavyochukuliwa. Kanuni ya 36(4) ya Kanuni za Bunge, inayoonesha mpangilio wa shughuli za Bunge, imetoa kipaumbele stahiki kwa masuala ya haki za Bunge.

Katika mpangilio huo, masuala ya haki za Bunge yamepewa nafasi ya kutangulia hoja nne. Hoja zinazotanguliwa ni hoja za Serikali, hoja za Kamati, hoja binafsi za Wabunge na shughuli nyingine yoyote ambayo Bunge litaona inafaa kushughulikiwa kwa wakati huo.

Kanuni ya 58 ya Kanuni za Bunge inafafanua utaratibu wa hoja kuhusu masuala ya haki za Bunge. Ufafanuzi huo unagusa mambo manne.

**Jambo la kwanza** linahusu sharti la Mbunge anayekusudia kuwasilisha hoja inayohusiana na haki za Bunge. Kanuni ya 58(1) ya Kanuni za Bunge inamtaka Mbunge huyo kuwasilisha suala hilo kufuatana na mpangilio wa shughuli za Bunge. Katika kufanya hivyo, Mbunge anayehusika atakuwa amekwisha mwarifu Spika mapema kuhusu kusudio lake na jambo ambalo anataka kuliwasilisha.

Kanuni ya 58(3) ya Kanuni za Bunge inasisitiza kuwa hoja hiyo ipewe kipaumbele katika kupanga shughuli nyingine zote za kikao kinachohusika. Msisitizo huo, unaonesha kuwa hoja inayoelezwa ni Hoja yenye hadhi maalumu.

**Jambo la pili**, ni wajibu alionao Mbunge aliyekwisha mwarifu Spika kuhusu suala la haki za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni ya 58(2) ya Kanuni za Bunge, Mbunge huyo atatakiwa kueleza sababu zilizomfanya aamini kwamba, suala lake linahusu haki za Bunge zilizotajwa kwenye Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge.

Masharti hayo yanasaidia kwa namna nne: **Mosi**, kutoa nafasi ya kuona iwapo hoja inakidhi vigezo. Kwa njia hiyo, Spika anapata fursa ya kujiridhisha kuhusu vigezo na masharti kabla ya kuiruhusu. Hii inamwezesha Spika kuona ustahiki wa hoja yenyewe.

**Pili**, kuhakikisha kuwa muda wa Bunge unatumika ipasavyo. Ikitokea Mbunge ameamini kuwa suala analowasilisha linahusu haki za Bunge, lakini Spika akabaini halihusu haki za Bunge, hoja hiyo inaweza kushughulikiwa kwa utaratibu stahiki. Kwa namna hiyo, muda wa Bunge utaweza kutumika mvizuri ambapo vinginevyo ingechukuliwa isivyostahili na kutumia muda vibaya.

**Tatu**, masharti hayo yanalenga kulinda uadilifu wa Bunge. Kwa jambo hili, Spika amepewa jukumu la kumtaka Mbunge aeleze sababu zinazomfanya aamini kuwa, suala lake linahusu haki za Bunge. Hii pia ni fursa kwa Spika kutathmini na kujiridhisha.

Kufanya hivyo ni njia ya kuliweka Bunge kwenye uadilifu katika uamuzi wake, kwa kuona kipaumbele kwa hoja kadri inavyostahili. Vinginevyo, uadilifu kwenye mpangilio wa hoja ungeweza kuwa hatarini katika sura ya kibunge.

**Nne**, masharti hayo yanaweka muktadha wa mwongozo au uamuzi wa Spika. Uamuzi huo ni kuhusu suala linaloelezwa na Mbunge kuwa linahusu haki za Bunge. Maelezo ya awali ya Mbunge kuhusu ukiukwaji au uvunjifu wa haki za Bunge, yanamsaidia Spika kuamua.

**Jambo la tatu** linaloelezwa katika Kanuni ya 58 ni kuhusu uamuzi wa Spika kumpa nafasi Mbunge kutoa hoja yake. Kanuni ya 58(3) inafafanua kuwa, iwapo Spika ataona kuwa suala la Mbunge linahusu haki za Bunge kuna mambo mawili ya msingi.

**Kwanza**, atampa nafasi Mbunge anayehusika kutoa hoja yake ambayo ni kuhusu haki za Bunge. Lengo ni kutoa fursa kwa Bunge kupata maelezo ya kina kuhusu suala kuu katika hoja. Ili Bunge liamue, linahitaji undani wa hoja. Hivyo ufafanuzi wa Mbunge unajenga hoja ipasavyo.

**Pili**, Kanuni ya 58(3) ya Kanuni za Bunge inasisitiza kuwa hoja hiyo ipewe kipaumbele katika kupanga shughuli nyingine zote za kikao kinachohusika. Msisitizo huo, unaonesha kuwa hoja inayoelezwa ni Hoja yenye hadhi maalumu.

**Jambo la nne,** ni kuhusu suala la haki za Bunge linaloibuka ghafla. Suala hilo kwa mujibu wa Kanuni ya 58(4) ya Kanuni za Bunge, litashughulikiwa kwa namna ambayo itafanya shughuli nyingine zilizokuwa zikiendelea, zisitishwe. Lengo bado ni kutoa kipaumbele kwa hoja zinazohusu haki za Bunge.

**Kanuni ya 36(4)**
**ya Kanuni za Bunge.**

**Inaeleza, kwa kawaida, hoja zinazohusu haki za Bunge zina sifa ya kutangulia kwa kipaumbele kabla ya hoja za Serikali, hoja za Kamati au hoja binafsi ya Mbunge kama ilivyoelezwa katika**

Kama ilivyofafanuliwa, Kanuni za Bunge la Tanzania zimetambua umuhimu wa kipaumbele kwa hoja zinazohusu masuala ya Haki za Bunge. Kwa ufafanuzi huo, hoja hizo zinapambanuliwa kwa namna kubwa tatu:

**Kwanza**, ni kutangulia kwa umuhimu ikilinganishwa na hoja nyingine. Utaratibu ni huo kwa suala linalozuka ghafla na kuonekana linahusu haki za Bunge. Kwa kawaida, hoja zinazohusu haki za Bunge zina sifa ya kutangulia kwa kipaumbele kabla ya hoja za Serikali, hoja za Kamati au hoja binafsi ya Mbunge kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 36(4) ya Kanuni za Bunge.

**Pili**, ni kutokufungwa na sharti la Kanuni ya 62(1) ya Kanuni za Bunge. Sharti hilo linataka hoja yoyote isitolewe Bungeni iwapo taarifa ya hoja hiyo haijawasilishwa kwa Katibu wa Bunge angalau siku moja ya kazi kabla ya Mkutano ambao hoja hiyo inakusudiwa kutolewa. Haiwi hivyo kwa hoja za kawaida za Serikali, za Kamati au hoja binafsi ya Mbunge isipokuwa kama Spika atatoa idhini yake kwa kutilia maanani udharura wa jambo linalohusika.

**Tatu**, kuzuia hoja inayoendelea ili kutoa nafasi kwa hoja nyingine. Kanuni za Bunge, zinaruhusu hoja kuhusu haki za Bunge izuie shughuli nyingine zilizo kuwa zikiendelea ili kupisha masuala ya haki za Bunge.

Kwa ujumla hoja zinazohusu masuala ya haki za Bunge katika Bunge la Tanzania, zimewekewa utaratibu kwenye Kanuni za Bunge. Utaratibu huo unazipa hoja hizo hadhi maalumu.

Msomaji anatafadhalishwa kumalizia kusoma kwa kuchukua mawazo ya mwanafalsafa wa kiingereza, John Locke aliyechangia pia uliberali duniani. Mwanafalsafa huyu anaamini kwamba, uimara wa demokrasia unategemea uwezo wake wa kulinganisha nguvu na haki maalumu zinavyopewa nafasi.

Vilevile yachukuliwe mawazo ya Mheshimiwa Winston Churchill aliyewahi kuwa Mbunge na Kiongozi wa Serikali ya Uingereza ambaye ana maoni kwamba, "Shughuli za Bunge lazima ziendeshwe kwa kuheshimu muda, kwani bila hoja ya kuahirisha, sauti ya watu inapotea katika mjadala usio na mwisho. "HADI TOLEO LIJALO LENYE UFAFANUZI ZAIDI."

# Bunge lapitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. **Deogratius Ndejembi** akizungumza Bungeni

Na. **Halima Laizer**

Moja ya majukumu ya msingi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kutunga sheria. Hili ni jukumu la kikatiba linalolifanya Bunge kuwa mhimili muhimu katika mfumo wa utawala wa nchi.

Kazi hii inatekelezwa kwa njia ya kujadili, kurekebisha, na hatimaye kupitisha miswada mbalimbali ambayo huwasilishwa na Serikali au Wabunge binafsi.

Sheria hizo hutoa msingi wa kiutawala, kuongoza taasisi, kulinda haki za wananchi, na kuweka misingi ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Katika utekelezaji wa jukumu hilo, Bunge huangalia mambo kadhaa, kuhakikisha sheria zinaendana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kurekebisha sheria zilizopitwa na wakati au zinazokinzana na mazingira ya sasa, kupitisha sheria mpya zinazolenga kuleta tija, uwazi, na maendeleo katika sekta mbalimbali na kusimamia utekelezaji wa sheria kwa kupitia Kamati za Kudumu za Bunge.

Katika Mkutano wa 19 wa Bunge la Bajeti mwaka 2025, Bunge limepitisha Miswada mbalimbali ya Marekebisho ya Sheria, hatua inayoonesha namna linavyotekeleza jukumu lake la msingi la kutunga sheria kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa taasisi za umma, kulinda rasilimali za taifa na kuendana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

> **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025** (*The National Housing Corporation [Amendment] Bill,* 2025) ambao uliwasilishwa Bungeni na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Deogratius Ndejembi, umelenga kuboresha Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa kwa kufanya maboresho ya kifungu cha 5 cha Sheria ya Shirika hilo, Sura ya 295.

Lengo kuu la marekebisho hayo ni kuondoa mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa sheria zilizopo, kuimarisha utendaji wa taasisi za umma, kuweka uwazi na uwajibikaji wa kiutendaji, sambamba na kwenda sambamba na mabadiliko ya kisera, kiuchumi na kijamii yanayoendelea nchini na duniani.

> **Katika hatua nyingine, Muswada huo pia unarejesha uwajibikaji wa moja kwa moja kwa wapangaji wa nyumba za Shirika.** Kwa mujibu wa marekebisho mapya, waajiriwa wa Shirika ambao wanatumia nyumba za Shirika sasa watalipa kodi ya pango kama ilivyo kwa wapangaji binafsi na inalenga kuongeza mapato ya Shirika

Mojawapo ya Miswada hiyo ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 (*The National Housing Corporation [Amendment] Bill,* 2025) ambao uliwasilishwa Bungeni na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Deogratius Ndejembi, ukilenga kuboresha Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa kwa kufanya maboresho ya kifungu cha 5 cha Sheria ya Shirika hilo, Sura ya 295.

Kifungu hicho cha 5 kimefanyiwa marekebisho ili kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa sheria hiyo, kwa kuongeza na kuboresha majukumu ya Bodi ya Shirika ambayo awali yalikuwa yanatekelezwa bila kutajwa kisheria.

Aidha, kifungu kipya cha 5A kimeongezwa ili kutoa mamlaka kwa Bodi kuunda kamati mbalimbali zitakazosaidia utekelezaji wa majukumu ya kiutawala na kiutendaji. Hii inalenga kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Shirika na kuwezesha mgawanyo bora wa kazi kwa kuzingatia taaluma na uzoefu wa wanakamati hao.

Kifungu cha 9 pia kimeongezwa na kurekebishwa ili kupanua wigo wa nyaraka ambazo Mkurugenzi Mkuu wa Shirika anaweza kukasimisha mamlaka ya kusaini kwa Maafisa Waandamizi wa Shirika. Kwa utaratibu uliokuwepo awali, Mkurugenzi Mkuu alikuwa na mamlaka ya kukasimisha usaini wa mikataba ya upangaji pekee. Kupitia marekebisho haya, Maafisa Waandamizi sasa wanaweza kusaidia kurahisisha mchakato wa usaini wa nyaraka nyingine muhimu, jambo litakalosaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa wakati na kwa ufanisi zaidi.

Katika hatua nyingine, Muswada huo pia unarejesha uwajibikaji wa moja kwa moja kwa wapangaji wa nyumba za Shirika. Kwa mujibu wa marekebisho mapya, waajiriwa wa Shirika ambao wanatumia nyumba za Shirika sasa watalipa kodi ya pango kama ilivyo kwa wapangaji binafsi na inalenga kuongeza mapato ya Shirika na kuimarisha ukusanyaji wa kodi, sambamba na kuimarisha uwajibikaji wa kila mpangaji.



Marekebisho ya kifungu cha 18 yanampa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya moja kwa moja ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika, tofauti na hapo awali ambapo uteuzi huo ulikuwa unafanywa na Waziri mwenye dhamana. Hatua hii inalenga kuimarisha utawala bora na kuongeza uwajibikaji katika usimamizi wa Shirika hilo muhimu la umma.

Aidha, kifungu kipya cha 18A kimeongezwa ili kutenganisha masharti yanayohusu uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na ajira za maafisa wengine wa Shirika, kwa lengo la kuweka mpangilio mzuri wa kisheria.

Muswada huo pia umeondoa dhana ya uwepo wa Mfuko wa Dhamana ambao hauna uhalisia wa kiutendaji, kwa kuwa hutoa tafsiri isiyo sahihi kwamba Shirika linatoa dhamana kwa wawekezaji binafsi, jambo ambalo si sahihi kisheria.

Aidha, marekebisho haya yatawezesha Shirika la Nyumba la Taifa kuwekeza kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370, ili kuhakikisha uwekezaji wa mashirika ya umma unazingatia viwango na matakwa ya kitaifa ya uwajibikaji wa fedha za umma.

Katika mkutano huo huo wa Bunge, pia ulipitishwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 (*The Written Laws [Miscellaneous Amendments] Bill, 2025*). Muswada huu umerekebisha sheria tisa muhimu ili kuimarisha mfumo wa kisheria nchini.

Miongoni mwa sheria zilizoguswa ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200 ambapo kifungu cha 26 kimeondolewa ili kuruhusu mashtaka kufunguliwa bila ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na ni hatua muhimu katika kuharakisha utoaji wa haki, kwani katika awamu zilizopita mashauri mengi yalihitaji ridhaa ya DPP kutokana na uhaba wa Mawakili wa Serikali nchini.

Sheria nyingine ni ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sura 177 imeboresha tafsiri ya neno "chemical" ili kujumuisha pia kemikali zinazotumika katika utengenezaji wa silaha za kikemikali, hatua itakayoongeza ufanisi katika uzuiaji na udhibiti wa vitisho vya kisayansi na kiusalama.

Pia, Sheria ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Sura ya 150, marekebisho yamefuta mamlaka ya Bodi katika kuteua wakuu wa idara, na kuweka mamlaka hiyo kwa Rais ili kuendana na dhana ya utawala bora. Aidha, kifungu cha 8 kimeboreshwa kuzingatia mamlaka ya nidhamu kwa mujibu wa sheria nyingine za utumishi wa umma.

Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Sura ya 59 imetanua tafsiri ya "medical research" ili kujumuisha tafiti za kuzuia magonjwa, kuimarisha ubora wa huduma za afya, na kujenga mifumo imara ya afya kwa jamii.

Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 imeboresha vifungu 3, 7B na 8B kwa kuondoa nafasi ya Naibu Mwandishi Mkuu wa Sheria na kuongeza jukumu la usimamizi wa Mikataba ya Serikali kwa Mwanasheria Mkuu, ili kuongeza tija katika utekelezaji wa Mkataba wa Serikali na kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

Sheria ya Bandari, Sura ya 166, maneno "security officer" yamebadilishwa kuwa "port security officer" ili kuendana na Kanuni za Kimataifa za Usalama wa Meli na Bandari (ISPS Code), huku kifungu kipya cha 60A kikianzisha Kamati ya Usalama wa Bandari, ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu usalama na hatari katika maeneo ya bandari.

> **Marekebisho haya yatawezesha Shirika la Nyumba la Taifa kuwekeza kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Msajili wa Hazina,** *Sura ya 370, ili kuhakikisha uwekezaji wa mashirika ya umma unazingatia viwango na* matakwa ya kitaifa ya uwajibikaji wa fedha za umma.

Kadhalika, Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317, imeondoa matumizi ya neno "uneconomic competition" na kulibadilisha kuwa "unfair competition" kwa lengo la kutumia msamiati unaoendana na mifumo ya soko huria ya kisasa. Pia marekebisho yamefuta misamiati kadhaa ambayo haina tena matumizi kwa mujibu wa mabadiliko yaliyofanyika, na kuongeza misamiati mipya kwa uwiano wa sheria ya sasa.

Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani**,** Sura ya 182 imeboreshwa ili kuweka uwazi katika matumizi ya kemikali, hasa katika mazingira ya makazi ya watu na maeneo ya viwanda, sambamba na kulinda afya ya jamii.

Pamoja na hayo, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413 imefanyiwa maboresho ya lugha na misamiati inayotumika katika utekelezaji wa majukumu ya mamlaka hiyo ili kuleta ufanisi na uwazi wa sheria kwa wadau wa usafiri wa ardhini.

Marekebisho ya sheria hizi ni hatua ya kimkakati inayolenga kuboresha utendaji wa sekta ya umma, kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji, kulinda usalama wa taifa, kuimarisha afya ya wananchi na kuongeza uwajibikaji katika taasisi za Serikali.

# Bunge Marathon Msimu wa Pili yavunja Rekodi




Na **Zuhura Mtatifikolo**

Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa amewashukuru wananchi kwa kuvunja rekodi ya kushiriki Msimu wa Pili wa mbio za Bunge Marathon ambazo lengo lake ni kukusanya fedha kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Jijini Dodoma.

Mbio hizo zilifanyika Aprili 12,2025 Jijini Dodoma na zilishirikisha wananchi, wadau na taasisi mbalimbali zikiwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo.

"Nawashukuru washiriki wote mliojitokeza kwenye Bunge Marathon leo, mmevunja rekodi kwa kukubali mwaliko kwenye mbio hizi za hisani, hiki ni kielelezo cha uzalendo.

"Nasikia faraja kwa kuwa washiriki wa rika mbalimbali wameshiriki mbio hizi kwa weledi mkubwa hadi vijana wadogo, ubunifu huu ni mzuri sana na unaunga mkono jitihada za Serikali za kujenga afya na mshikamano," alisema.

Alisema kwa upande mwingine fedha zinazokusanywa kupitia Bunge Marathon zitasaidia kujenga Shule ya Wavuala ya Kidato cha Sita katika eneo la Kikombo Jijini Dodoma kwa gharama ya shilingi bilioni tatu.

"Kupitia mbio hizi tunaamini jamii italiunga mkono Bunge ili

> **Kupitia mbio hizi tunaamini jamii italiunga mkono Bunge ili malengo haya yafikiwe na ninawahakikishia kwamba fedha yote iliyotolewa itakwenda kufanya kazi iliyokusudiwa.**
>
> *Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa*




malengo haya yafikiwe na ninawahakikishia kwamba fedha yote iliyotolewa itakwenda kufanya kazi iliyokusudiwa.

"Pongezi kwa Mheshimiwa Spika kwa ubunifu huu, shule itakuwa na vyumba vya madarasa vya kutosha, maabara nne za kisasa, maktaba, mabweni ya wanafunzi 300, bwalo la chakula, viwanja vya michezo na nyumba za walimu," alisema.

Alisema juhudi hizo zinaenda sambamba na kazi zinazofanywa na Serikali za kuongeza idadi ya shule za msingi kutoka 16,656 mwaka 2020 hadi kufikia 19,783 mwaka jana na kwa sekondari 5,001 mwaka 2020 mpaka kufikia 5,526 Desemba mwaka jana.

Aidha, alisema Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa shule maalumu za wasichana zilizojengwa katika kila mkoa kwa gharama ya shilingi bilioni 116 ambapo Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameendelea kufungua fursa mbalimbali.

Alieleza kuwa shule hizo zitaimarisha mkakati wa kufundisha TEHAMA na baadhi ya shule zitakuwa za amali ili kutoa ujuzi stahiki ili ziweze kusaidia kuongeza uelewa kwa wanafunzi.

"Serikali imeongeza bajeti ya elimu ya juu na elimu ya kati kwa lengo kuimarisha zaidi elimu na kuhakikisha kila kitu kinaenda vizuri kwa sababu inaelewa umuhimu wa elimu,"alisema Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu alilishukuru Bunge pamoja na wafadhili mbalimbali waliotoa fedha na vifaa kwa ajili ya kuendesha mbio hizo.

**Spika: Hizi ni mbio za wananchi**

Awali, Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson alisema mbio hizo zimejumuisha wabunge zaidi ya 264 wakiwemo wanaotoka katika majimbo mbalimbali pamoja na wananchi na kwamba ndizo mbio pekee za wananchi.

"Hii ndio marathoni pekee ya wananchi tukisema wananchi naona Hersi (Rais wa klabu ya Yanga) ananiangalia, na wenye nchi (Simba) msiwe na wasiwasi na ninyi ni sehemu ya wananchi hivyo nawashukuru sana kwa kuja," alisema Dkt. Tulia

Alisema Bunge limeamua kuunga mkono Serikali kwa kujenga shule ya wavulana ambapo wamefanya hivyo ili wawe




> **Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bunge Marathon, Mheshimiwa Festo Sanga alisema Bunge Marathoni inafanyika kwa mara ya pili ambapo mwaka jana walisajili zaidi ya wakimbiaji 3,000 lakini mwaka huu wamejitokeza zaidi ya wakimbiaji 4,000.**

mfano mzuri wa kuhakikisha elimu inapatikana bila kuwa na ubaguzi wowote.

Mheshimiwa Dkt. Tulia alisema ujenzi wa shule hiyo utakuwa jirani na shule ya wasichana ambayo ilijengwa na Bunge katika eneo la Kikombo jijini Dodoma ili Wabunge na Bunge wapate nafasi ya kuingalia kwa ukaribu.

"Tanzania inajengwa na wa kiume na wa kike, Mbunge Mavunde (Mbunge wa Dodoma Mjini) tunakuletea shule hizi mbili lakini nitumie nafasi hii kukupongeza sana kwa kazi nzuri unayoifanya kwa wana Dodoma," alisema.

Aidha, anasema lengo lingine la mbio hizo ni kufanya mazoezi kwa ajili ya kujikinga na magonjwa ambayo sio ya kuambukiza pamoja na kuiunga mkono kwa vitendo ikiwemo kauli ya Rais Samia ya ufanyaji wa mazoezi.

"Sisi Bunge tumelichukua kwa umuhimu ndio maana kila Bunge tunafanya bonanza ili kuiweka miili yetu vizuri na kupitia marathoni hii tunaweka miili vizuri kwa kufanya mazoezi hivyo tunakuwa tumemuunga mkono Mheshmiwa Rais," alisema

### Zaidi ya wakimbiaji 4000

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bunge Marathon, Mheshimiwa Festo Sanga alisema Bunge Marathoni inafanyika kwa mara ya pili ambapo mwaka jana walisajili zaidi ya wakimbiaji 3,000 lakini mwaka huu wamejitokeza zaidi ya wakimbiaji 4,000.

"Tunashukuru wote walioshiriki mbio hizi zimekuwa na faida kubwa mno kwetu kwa sababu tumefanya mazoezi na dhamira yetu ya ujenzi wa shule inaenda kutimia kwa vitendo," alisema Mheshimiwa Sanga.

### Mbio zimekuwa na ubora

Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma alisema mbio za mwaka huu zimekuwa na ubora wa hali ya juu na kwamba Wizara yake itaendelea kuhamasisha Watanzania kufanya mazoezi ili kujikinga na magonjwa ambayo siyo ya kuambukiza.

Katika mbio hizo, Mwanariadha mashuhuri nchini, Gabriel Geay aliibuka kinara katika mbio za kilomita 10 zilizokuwa na ushindani akitumia muda wa dakika 28:04 akimshinda mshindani wake Benjamin Fernandez ambaye alitumia muda wa dakika 28: 19 huku mshindi wa tatu akiwa ni Sinda Daniel aliyetumia muda wa dakika 28: 23.

Mbio hizo zilikuwa za aina yake kutokana na watu mbalimbali wa kila rika kujitokeza wakiwamo watoto, wazee, vijana na Wabunge na Mawaziri mbalimbali.

### Geay ageuka kivutio

Mwanariadha mkongwe nchini Geay ambaye ni mshindi wa pili wa mashindano ya Boston Marathon aligeuka kivutio katika mbio hizo kutokana na ubora wake wa kukimbia ambapo mara baada ya mbio hizo kumalizika baadhi ya wanariadha chipukizi walikuwa wakiomba kupiga naye picha.

"Nashukuru Mungu nimepata ushindi lakini ushindani ulikuwa mkubwa pia hali ya hewa haikuwa rafiki, tumezoea kukimbia maeneo yenye baridi kama Arusha,"alisema mwanariadha huyo.





E MARATHON
1
2
3




START
Shiriki Michezo kwa Maendeleo ya Taifa Letu




Jarida hili limeandaliwa na: Ofisi ya Bunge, 10 Barabara ya Morogoro  S.L.P. 941, 40490 Tambukareli, DODOMA.
Nukushi: +255 26234218 Simu: +255 26 232276-5 Barua Pepe: cna@bunge.go.tz